# Nipashe

Jumatatu Machi 20, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581255

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII



The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11


SUPA JACKPOT

TZS. 1,090,583,531

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#




## EATV Kinara yawatambua wanawake 8

UKURASA 3

### MIAKA 2 YA SAMIA

# Samia: Nilibezwa sasa ninakubalika

• **Katiba** mpya... asema kila jambo linakwenda kwa... *Ukurasa 2*




Rais Samia Suluhu Hassan akihutubia wananchi katika sherehe za kilele cha Miaka Mawili ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita iliyoandaliwa na Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Ahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa mauaji ya kianzio cha 100,000/-

UKURASA 3



Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Suzan Lyimo (kushoto), akiwa na Getrude Mongela ambaye ni mwanasiasa maarufu wa CCM wakielekea kwenye viti wakati wa sherehe za miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan zilizoandaliwa na Umoja wa Wanawake wa CCM katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Alivyopambana na mamba dakika 45

UKURASA 5


**MICHEZO** CHAMA KINARA WA MABAO CAF UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Samia: Nilibezwa sasa ninakubalika

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema pamoja na mafanikio yanayoonekana sasa nchini, anakumbuka namna alivyoingia madarakani kwa kubezwa kutokana na dhana miongoni mwa jamii kuhusu jinsia ya kike, kwamba inaweza kufanya kazi ipasavyo na kuleta mabadiliko.

Aidha, amesema kwa kipindi cha miaka miwili, kipekee anawashukuru wanaume ambao nao wamefanikisha hatua za kimaendeleo zilizopigwa nchini, kipindi ambacho amefanya kazi nzuri na kubwa na tafsiri hiyo inajionyesha wazi.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, kwenye sherehe ya kumpongeza kutimiza miaka miwili tangu aingie madarakani Machi 19, mwaka 2021 zilizoandaliwa na Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT).

Kadhalika, sherehe hizo zilihudhuriwa na viongozi na wanachama wa Baraza la Wanawake CHADEMA (BAWACHA), zilizofanyika Uwanja wa Uhuru, jijini humo.

Katika hotuba yake ilichukua takribani dakika 40, Rais Samia alijikita zaidi kuzungumzia mafanikio, changamoto zinazomkabili mwanamke wa Kitanzania, akisisitiza kwamba mwanamke anapopewa nafasi na kupewa nguvu anaweza.

“Tulipoanza mwaka 2021 bezo lilikuwa kubwa, lakini bezo...unapobezwa unajenga ujasiri na kazi inaendelea. Nawashukuru wanawake kwa kunipa nguvu, nguvu kwa kuwa nimeweza. Pongezi hizi ziende kwa wanawake Watanzania wote,” alisema Rais Samia.

**MIRADI KIMKAKATI**

Alisema, wakati anaingia madarakani aliikuta miradi ya kimkakati iliyoanzishwa na mtangulizi wake, Hayati John Magufuli, ikiwamo ya ujenzi wa reli ya kisasa na barabara na ambayo amehakikisha inaendelea kutekelezwa ipasavyo, ili kuifungua kiuchumi nchi barani Afrika na duniani.

“Niliahidi kuzitekeleza kazi za mwenzangu na mpaka sasa hakuna kilichosimama, kwa pamoja tumshukuru Mungu. Lengo la kuanzisha Wizara ya Jamii, ni kumsogeza mwanamke kutoka aliko na kupunguza unyanyaji wa wanawake na watoto,” alisisitiza Rais Samia.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili hazikukosekana changamoto hasa zikichangiwa na mambo kadhaa kama vile vita nchini Ukraine, Uviko-19 pamoja na mabadiliko ya tabianchi, ambayo yanasababisha chakula kisizalishwe kwa wakati.

“Changamoto hizi zinasababisha bei za chakula zipande, adimu, niwahakikishie wananchi kama tulivyofanya kwenye mafuta (petroli/dizeli) na kuweka ruzuku ya Sh. bilioni 100, ili bei ziwe za wastani, ndivyo tumechukua hatua sekta nyingine,” alisema Rais Samia na kuongeza:

“Hata katika mbolea, tulitoa ruzuku na serikali ilichukua hatua kupunguza makali ya uchumi, ili Watanzania kuwa na ustawi mzuri. Mkutano wa mapinduzi ya kijani katika ukanda wa Afrika Mashariki unatisha, ila Tanzania bado tuko vizuri. Fedha za kigeni, Tanzania bado iko vizuri.’

“Ndugu zangu kuna changamoto kubwa moja ambayo huwa hatuizungumzii, tunasema ajenda ya wanawake ni moja, lakini tunapokuwa kwenye siasa tunagawanyika. Sisemi wote tuwe na itikadi moja...yanayomsibu mwanamke wa Kitanzania lazima tuyasemee.

“Manyanyaso yanayotokea kwenye siasa vyama, lazima tuseme, tubadilike, tunaposimama majimboni tuungwe mkono na si kusimamishwa kimtego mtego, kwa ambayo yanayotuhusu tusimame pamoja.”



**KATIBA MPYA**

Kuhusu Katiba mpya, Rais Samia alisema nia ipo, ndiyo maana akafungua milango ya mazungumzo ikiwamo maridhiano, akiamini kila japo linakwenda kwa hatua.

“Tumesema Katiba mpya, tunataka ibadilike tumesema sawa, kila jambo ni kwa hatua kwa hatua, sifa ya Tanzania ambayo tumeijenga kwa utawala bora lazima tuijenge. Mimi kama mwanamke najiamini, sifa ya mwanamke ni kujiamini, nimefungua uwanja wa siasa, CCM nikiamini tuko pamoja na tutajadiliana kwa pamoja,” alisema.

Aidha, katika kumkwamua mwanamke na vikwazo vya kiuchumi, kwenye sekta mbalimbali, alisema serikali yake ilipounda Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, lengo ni kuiinua jinsia hiyo.

“Wanawake ni wajasiriamali wanaouza bidhaa mbalimbali ndani na nje ya nchi. Tanzania ni lazima tuwe mabingwa kusimamia mwanamke kukuzwa kiuchumi, lazima nionyeshe kivitendo, ndani ya nchi yangu nasimamia mwanamke kukuzwa kiuchumi.”

“Tunataka masoko ambayo yanaweza kumfanya (mwanamke) akafanya shughuli zake na kumlea mtoto wake. Nataka kuonyesha kwa vitendo,” alisema Rais Samia.

**USAWA 50/50**

Kadhalika, alisema ili kufikia lengo la 50/50 kwenye nafasi ya mwanamke katika uongozi, kuna ongezeko la nafasi za wanawake kiuongozi akitaja Mahakama Kuu ina majaji 86 kati yao 40 ni wanawake na maofisa tawala wa mikoa 26 kati yao 12 ni jinsia hiyo huku bungeni akisema bado kuna kazi ya kufanya.

“Bungeni nako tunakwenda polepole kama sio 50 basi asilimia 40 tujitokeze kwa wingi kwenye uchaguzi. Wanawake ajenda yetu ni moja, sasa tutakwenda kwa awamu mwaka huu wameanza BAWACHA (Baraza la Wanawake wa Chadema) kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, mwaka kesho ACT-Wazalendo.”

Alisema serikali yake imejikita kumkwamua Mtanzania kiuchumi, kutokana na Ilani ya CCM, akisema kaulimbiu ya mwaka huu ya siku ya Wanawake Duniani; Teknolojia na Ubunifu ndio msingi wa maendeleo, iwe msingi wa maendeleo.

“Hatujayamaliza yapo yanayokosesha huduma wanawake, lakini katika elimu tunakwenda kujenga shule za sayansi kwa wasichana kwenye kila mikoa na VETA (Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi), kila wilaya, ili wawe wabunifu.”

Kuhusu sekta ya afya, Rais Samia alisema maboresho yanaendelea na kuhusu mfumo wa M-MAMA unaolenga kunusuru vifo vya wanawake wanaojifungua tayari umeokoa maisha ya mama na mtoto.

Vilevile, katika sekta ya kilimo, Rais Samia alisema kutokana na kilimo kuajiri zaidi vijana, serikali yake imeanzisha shamba litakaloahusisha vijana ambalo linazinduliwa leo (Machi 20, mwaka huu) jijini Dodoma.

“Teknolojia inasaidia kuokoa muda, miundombinu bora ya anga na nchi kavu, reli, barabara inasaidia Watanzania kuchukua muda mfupi. Dar es Salaam yote imejaa vumbi, kazi inaendelea, Dodoma nako inaruka vumbi kurahisisha usafiri.

“Katika bandari pia tunajenga bandari zetu, ili kurahisisha biashara ndani ya bara la Afrika. Tuliachiwa miradi mikubwa miwili ya kimkakati na kazi inakwenda, itaongeza tija kwa shughuli za kijamii na kiuchumi,” alisema Rais.

Kadhalika, kuhusu mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na kila halmashauri nchini, takwimu inaonesha iliyokopeshwa kwa asilimia 88 fedha hazijarejeshwa hivyo kuna haja ya kufuatilia suala hilo.

Katika mkutano huo wanawake wa vyama vya upinzani vya ACT-Wazalendo na CHADEMA walihudhuria.

HABARI KITAIFA

# EATV Kinara 2023 yawatambua wanawake 8

Na Romana Mallya

KAMPENI ya EATVKinara2023 imewatambua na kuwapatia vyeti wanawake mashujaa wanane, ambao hawaonekani ndani ya jamii, lakini wanafanya mambo makubwa.

Vyeti hivyo vilitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa EATV na East Africa Radio, Regina Mengi katika hafla iliyofanyika juzi jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wadau katika sekta mbalimbali ambao pia walishiriki mijadala iliyoendeshwa siku hiyo mbashara.

Mijadala hiyo iliendeshwa na watangazaji wa kituo hicho ilibebwa na mada mbalimbali zikiwamo uhuru wa kiuchumi, mikopo, uwekezaji na akiba, mwanamke na teknolojia, uzazi wa mpango unavyochangia katika kukuza uchumi wa familia.

Mratibu wa Vipindi EATV and Redio, Irene Tillya, alisema ni mwaka wa pili mfululizo kwa EATVKinara kuwatambua wanawake katika biashara, ujasiriamali na jamii kwa ujumla.

Pia kuwaibua mashujaa ambao hawaonekani kwenye jamii, lakini wanafanya makubwa.

"Walengwa ni wanawake wenye umri kati ya miaka 25 hadi 50, ambao ni wajasiriamali wanafanya kazi katika biashara za ushirika, mwaka jana jumla ya mashujaa 10 tuliweza kuwaibua na kuwatambua na tayari wamefunguliwa fursa ndani na nje ya Tanzania," alisema.

Alisema tukio hilo limekuwa na linaendelea kukua kwa wajasiriamali kuonyesha biashara zao na kupata ujuzi kupitia makongamano mbalimbali ambayo hutokea kila wakati.

"Ninawashukuru nyote mmetusaidia kwa ukaribu na kutuunga mkono kwa dhima kuu ya EATVKinara, ili kufikia mafanikio, washirika wetu ni Konyagi, TBL, Benki ya NMB, Trust Daisy na kampuni ya maji ya Kilimanjaro," alisema.

Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF), Anna Kulaya, akichangia mada ya mwanamke na teknolojia na namna inavyoweza kutumika kutafuta masoko, alisema bado mwitikio wa mwanamke katika hilo ni mdogo ikilinganishwa na wanaume.

"Mfano, katika mtandao wetu wa shirika, wengi wanaoutembelea ni wanaume, ukirudi katika jamii wanawake bado wanaogopa kutumia mtandao kwa hofu ya kudhalilishwa au kuharibiwa biashara wanazofanya.

"Ni lazima elimu iende kwao ili watumie hizi fursa, teknolojia ibebe majukumu yao na wao waweze kujikwamua kiuchumi," alishauri.

Mkurugenzi Mtendaji wa Jamii Forum, Maxence Mello, alisema teknolojia ina fursa na haijalishi jinsia ya mtu.

Mello alimpongeza Regina Mengi kwa kuona umuhimu wa kuwatambua wanawake wanaofanya makubwa ndani ya jamii.

Kampeni ya EATVKinara imewatambua wanawake wanaojishughulisha na kazi mbalimbali ndani ya jamii katika sekta tofauti wanaotoka mikoa tofauti. Walioibuliwa na kupewa vyeti ni Lydia Kivinge kutoka Iringa anayejishughulisha na kilimo, Mwanahamisi Nyagali kutoka Lindi mshonaji wa nguo, Cecilia Cholela kutoka Dodoma anayefanya kazi ya uuzaji wa mbao na matofali.

Wengine ni Tarsila Faustin kutoka Mwanza ambaye ni mbunifu wa taulo za kike na mashine ya kuchomea taulo za kike (pads), Editrudith Lukanga (EMEDO) kutoka Mwanza ambaye ni mwanzilishi wa Shirika la Kusaidia wavuvi wadogo wanawake.

Linda Solomon kutoka Arusha, ni fundi magari, Emaculata Peter kutoka Dar es Salaam anayejishughulisha na ufundi wa kupaka rangi nyumba na Hadija Garasia kutoka Rukwa mfanyabiashara wa chakula.




Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande, akitoa maelezo ya mradi wa kituo cha upanuzi cha kuzalisha umeme kwa gesi asilia cha Kinyerezi I, mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, iliyotembelea kujionea utekelezaji wa shughuli mbalimbali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ujenzi kituo kupoza umeme wafikia 59 %

Na Neema Mbuja, CHALINZE

UJENZI wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Chalinze mkoani Pwani, umefikia asilimia 59 huku njia ya kusafirishia umeme mkubwa wa kilovoti 400 kutoka Bwawa la Mwalimu Nyerere ukifikia asilimia 92.

Meneja Mradi wa Kituo cha Kupokea na Kupoza Umeme Chalinze, Mhandisi Newton Livingstone, aliieleza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyotembelea mradi huo mwishoni mwa wiki.

Alisema mradi huo unajumuisha miradi miwili ambayo ni njia ya kusafirisha umeme mkubwa kutoka Bwawa la Nyerere chenye urefu wa kilomita 160 wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 51.5 na Sh. bilioni 39.12.

Pia ujenzi wa kituo hicho kwa thamani ya dola za Marekani milioni 44.06 na Sh. bilioni 30.85 kitakachohusisha ufungaji wa mashine sita zenye uwezo wa megavoti 250 kila moja. Baada ya kutembelea mradi huo, akizungumza wakati wa majumuisho, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dustan Kitandula, alieleza kuridhishwa na utekelezaji wa mradi huo ambao unakwenda sambamba na ujenzi wa Bwawa la Nyerere.

Aidha, Kamati hiyo imeitaka Wizara ya Nishati na TANESCO kukamilisha kwa wakati miradi miwili kabla ya kukamilika kwa mradi wa JNHPP mwakani.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa majumuisho ya ziara ya kamati hiyo kutembelea miradi ya maendeleo.

Alisema kamati imeridhishwa na utekelezaji wa miradi hiyo na kuongeza kuwa itasaidia katika uwekezaji mkubwa na kukuza uchumi wa nchi yetu.

"Uchumi wa nchi unakuwa kwa kasi sana sambamba na mahitaji ya upatikanaji wa umeme hivyo TANESCO hakikisheni mnaweka msukumo mkubwa kwenye miradi hii," alisema Kitandula.

# Ahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa mauaji ya kianzio cha 100,000/-

Na Joctan Ngelly, GEITA

MAHAKAMA Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita, imemhukumu Emmanuel Mbuga (36) kunyongwa hadi kufa kwa kosa la kokodi watu na kumuua Simon Ndege kwa kumchoma sururu tumboni hadi utumbo kutoka nje.

Mshtakiwa huyo alidaiwa kukubaliana na wauaji malipo ya Sh. 1,000,000 na kuwalipa Sh. 100,000 kama kianzio ili wakitimiza kazi hiyo awalipe Sh. 900,000 zilizobaki.

Hukumu hiyo imetolewa na Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Ntemi Kilekamajenga, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo.

Jaji alisema mahakama hiyo imetoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa ili iwe fundisho kwake na watu wengine wenye tabia za kikatili kama yake.

Alisema upande wa mashtaka ulipeleka mahakamani mashahidi saba na vielelezo vitano ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo kwa kukusudia.

Jaji Kilekamajenga alisema washtakiwa katika kesi hiyo ni Erasto Simoni (63) na Emmanuel Mbuga (36) ambao walikuwa wanatetewa na mawakili wawili wa kujitegemea Forgeth Mongi na Martha Nicliolaus.

Jaji Kilekamajenga alisema mshtakiwa wa kwanza Simoni alikuwa na mgogoro wa ardhi na Yanga Ndege na alikuwa akimtuhumu kuwa ni mchawi kwa madai ya kumroga binti yake.

Alisema baada ya tuhuma hizo mshtakiwa alikodi watu wawili, mshtakiwa wa pili Emmanuel Mbuga na mwenzake ambaye alifariki dunia, kwa Shilingi milioni moja ili kumuua Ndege.

Jaji Kilekamajenga alisema Oktoba 5, 2019 majira ya usiku katika Kijiji cha Mgusu washtakiwa walivunja mlango wa nyumba na kuingia ndani kwa lengo la kumuua Ndege, lakini walikosea na kumuua mdogo wake Simoni Ndege kwa kumchoma na sururu tumboni na utumbo kutoka nje na kufariki dunia papo hapo.

Alisema baada ya mauaji hayo walikimbia na kutokomea kusikojulikana, na Ndege ambaye ni kaka wa marehemu alipiga kelele za kuita majirani na kutoa taarifa kwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Mgusu.

Alisema, Mwenyekiti alipofika eneo la tukio alimuuliza kaka wa marehemu kama anawatambua waliomuua mdogo wake na kujibu kuwa anawatambua kwa sura kwa kuwa hawakuficha sura zao na walikuwa na nondo pamoja na sururu walizotumia kumchoma mdogo wake tumboni na utumbo kutoka nje.

Jaji Kilekamajenga alisema kuwa ameangalia ushahidi wa pande zote na kugundua kuwa mshtakiwa wa kwanza, upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha kosa na mahakama kumwachia huru.

Aidha, mshtakiwa wa pili Emmanueli Mbuga (36) upande wa mashtaka umethibitisha kosa pasipokuacha shaka na kumtia hatiani kwa kosa la mauaji ya kukusudia.

Jaji Mfawidhi Kilekamajenga, alisema mahakama inamhukumu mshtakiwa huyo kunyongwa hadi kufa na haki ya rufani ipo wazi.

# HABARI PICHANI



Mkurugenzi wa Kituo cha Radio na Televisheni cha EATV, Regina Mengi (kulia), akimkabidhi cheti cha shukrani mwakilishi wa Kampuni ya Maji ya Kilimanjaro, Neema Mangowi, kutokana na kampuni hiyo kudhamini kongamano la EATV Kinara kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA ZOTE: JUMANNE JUMA**



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WILDAF), Anna Kulaya (kushoto), akitoa hoja wakati wa kongamano la Mwanamke Kinara lililoandaliwa na EATV ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.



Baadhi ya wanawake wakiwa katika kongamano.



Mmoja wa wafanyakazi wa EATV akichangia mada katika kongamano.



Mmoja wa washiriki akitoa mchango wake kwenye kongamano hilo.



Sehemu ya washiriki wakifuatilia mada mbalimbali.

HABARI KITAIFA

# Asimulia alivyopambana na mamba dakika 45

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Kata ya Rutamba, Manispaa ya Lindi, Salum Kindamba (44), amelazwa Hospitali ya Rufani Sokoine mkoani Lindi baada ya kushambuliwa na mamba wakati akivua samaki na wenzake katika eneo la Bwawa la Katani, Kata ya Rutamba.

Tukio hilo lilitokea Machi 11, mwaka huu, majira ya saa 9:00 usiku wakati Kindamba na wavuvi wenzake wakiwa wanavua samaki.

Akisimulia mkasa huo hospitalini hapo, Kindamba alisema akiwa na wavuvi wenzake waliondoka nyumbani majira ya jioni ili wakavue samaki kwa ajili ya kujipatia kipato na kitowewo.

Kindamba ambaye amejeruhiwa na mamba huyo maeneo ya kifuani, bega la kushoto, tumbo na kushonwa nyuzi, usoni, shavuni na kidevuni, alisema akiwa anatega nyavu ndani ya bwawa hilo, mamba aliyekuwa mawindoni alimvamia na kumng'ata mkono wa kushoto eneo la bega.

Alisema wakati mamba akijaribu kumvuta kwenye maji ya kina kirefu, alijihaki kwa kutumia mkono wake wa kulia kumpiga mamba ngumi ya kichwa na kumwachia kisha kuondoka zake, hata hivyo, alisema alirejea tena na kumng'ata sehemu zingine za mwili wake, hali iliyomfanya atumie mkono wake mwingine kumpiga ngumi kwenye pua.

Aliendelea kusimulia kuwa baada ya ngumi hiyo alimwachia, lakini alimrudia tena na kumng'ata mikono yote miwili na kujaribu kumvuta kwenye maji yenye kina kirefu, ndipo mvuvi huyo alipojihami kwa kutumia kichwa chake kumpiga mamba huyo, ambaye hatimaye alimwachia na kuondoka zake.

"Ilinichukua dakika 45 kuanzia saa 9:05 usiku hadi 9:55 naendelea kupambana na mamba aliyekuwa amenivamia," alisema Kindamba.

Alisema baada ya mamba huyo kumwachia, wavuvi wenzie walimfuata na kumpakia kwenye mtumbwi waliokuwa wanavulia samaki na kumkimbiza Kituo cha Afya Rutamba kwa ajili ya matibabu na baadaye kuhamishiwa hospitalini humo.

Mganga Mfawidhi Hospitali ya Sokoine, Dk. Godwin Macheku, alithibitisha kumpokea mvuvi huyo akiwa katika hali mbaya, lakini baada ya matibabu alisema anaendelea vizuri.

## Mahakama yaahirisha uchunguzi mtuhumiwa aliyefia mahabusu

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kinondoni, Kivukoni Dar es Salaam, imeahirisha kufanyika kwa uchunguzi wa chanzo cha kifo cha mfanyabiashara Stella Moses aliyefia mahabusu ya Kituo cha Polisi Mburahati mwaka 2020 hadi itakapopitia nyaraka halisi za maelezo ya mashahidi.

Hata hivyo, Wakili wa waleta maombi hayo, Peter Madeleka, aliwasilisha kwa mdomo taarifa ya kukaa rufani kupinga uamuzi huo mdogo kwa sababu anaona mahakama hiyo haiwatendei haki wateja wake.

Uamuzi huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Hakimu Mkazi Mfawidhi, Franco Kiswaga, baada ya kupitia hoja za pande zote mbili na maoni ya washauri wa mahakama (wazee wa baraza) kuhusu pingamizi lililowasilishwa na upande wa wadaiwa na nyaraka mpya katika shauri hilo.

"Baada ya kusikiliza maelezo ya pande zote mbili na kupata maoni ya washauri, mahakama inaona ni busara iahirishe huu uchunguzi ili iweze kuzipitia hizo nyaraka ambazo ziliwasilishwa mahakamani," alisema Kiswaga.

Pia, aliagiza nyaraka hizo halisi ziwasilishwe mahakamani Jumatano ya wiki ijayo (Machi 22) ili mahakama iweze kuzipitia, kwa sababu nyaraka zilizokuwa zimewasilishwa zilikuwa ni nakala.

Baada ya Hakimu Kiswaga kutoa uamuzi, huo Madeleka aliieleza mahakama kuwa anatoa taarifa ya mdomo ya kukata rufani kwa sababu hawajakubaliana na hawajaridhika na uamuzi huo.

"Tunaona tunapoteza muda katika mahakama hii ni bora twende mbele katika Mahakama Kuu ili wateja wangu waweze kupata haki yao, leo hatukuja kuchunguza nyaraka, tulikuja kuanza kuchunguza chanzo cha kifo cha Stella," alidai Madeleka.

Awali, Hakimu Kiswaga alisema shauri hilo lilipokuja Machi 9, 2023 wakili wa wajibu maombi, Job Mrema, aliomba uchunguzi usiendelee na kuomba kutumia jalada jipya aliloleta, lakini wakili wa waleta maombi alipinga.

Alisema hoja ambayo mahakama imejenga inaona kwa kuwa tayari shauri la mwanzo lilikuwa limeshafunguliwa na hakuna kifungu chochote walichokiacha kwa hiyo mahakama inalitupilia mbali pingamizi la Mrema. Baada ya uamuzi huo, Wakili Madeleka aliomba mahakama ihamie Kituo cha Mburahati ili kuona namna tukio lilivyofanyika na wanapokuwa huko anaomba kupitia nyaraka za polisi zinazoendesha kumbukumbu za taarifa za kituo hicho ili kujua askari aliyekuwa zamu siku hiyo.

Akijibu hoja hizo, Wakili wa wajibu maombi, Flora Massawe, akisaidiana na Mrema alidai kuwa hoja zilizowasilishwa na wakili hazijakamilika kwa hatua hiyo, kwa maana anapoomba mahakama kwenda kituo cha polisi ili kuona tukio lilivyofanyika na kuomba mahakama ipitie kwanza nyaraka.

Stella alifariki dunia usiku wa Desemba 20, 2020, akiwa mahabusu ya Kituo cha Polisi Mburahati alikojisalimisha baada ya kupata taarifa kuwa alikuwa anahitajika, huku polisi ikidai mtuhumiwa huyo alijinyonga.


MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

### TANGAZO KWA UMMA

**Utaratibu wa Kushughulikia Uingizaji wa Mizigo Nchini kwa Utaratibu wa Kuchangia Makasha "Cargo Consolidation & De-Consolidation"**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwakumbusha wananchi kwa ujumla na waagizaji wa mizigo kutoka nje ya nchi kupitia utaratibu wa kuchangia Makasha (Containers) ujulikanao kama "Cargo consolidation & De-consolidation" kwa kutumia mawakala wanaofanya shughuli hizi, juu ya umuhimu wa kuzingatia **Sheria, Kanuni na Taratibu** zinazosimamia utaratibu huo kama zilivyoainishwa kwenye sheria na kanuni; ***The Tanzania Shipping Agencies (Cargo Consolidator and De-Consolidator Regulation), G.N. No. 337 of 2018" hususani kifungu Na. 4 (1) (b), (c) na (m).***

Ni takwa la kisheria kwa mwagizaji wa mzigo anayetumia utaratibu huu kuhakikisha yafuatayo:-

**(i)** Wakala atakayemtumia kusafirisha mzigo wake ana leseni hai ya uendeshaji wa shughuli za "Cargo Consolidation & De-consolidation" inayotolewa na Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC) kabla ya kuanza kufanya naye biashara,

**(ii)** Anatumia Wakala wa Forodha mwenye Leseni hai inayotolewa na TRA kupitia kwa Kamishna wa Forodha na Ushuru wa Bidhaa,

**(iii)** Wakala wa Usafirishaji (Consolidator) anatoa nyaraka za kusafirisha mizigo kwa kila mchangiaji kwenye Kasha husika. Nyaraka hizi ambazo zinajulikana kama House Bill of Lading ndizo zitakazotumika kugomboa mizigo ya kila mchangiaji,

**(iv)** Anapata risiti sahihi ya huduma ya kusafirisha mizigo (EFD) kutoka kwa Wakala wa Usafirishaji pamoja na risiti ya huduma ya kugomboa mizigo bandarini ambayo inatolewa na Wakala wa Forodha.

Kwa upande wa Consolidators na De-Consolidators, wazingatie yafuatayo:-

**(i)** Kuhakikisha anafuata matakwa ya sheria tajwa hapo juu ambayo ni pamoja na kuwasilisha leseni yake ya uwakala wa usafirishaji (Consolidation & De-consolidation) kwa Kamishna wa Forodha na Ushuru wa Bidhaa ili kukamilisha taratibu za kiforodha,

**(ii)** Kuhakikisha anakuwa na nyaraka kuu ya kusafirishia mizigo husika (Master Bill of Lading),

**(iii)** Anawapatia wamiliki wa mizigo nyaraka husika ili waweze kugomboa mizigo yao bila usumbufu baada ya kuwasili bandarini,

**(iv)** Kutimiza wajibu mwingine wowote kwa mujibu wa sheria za kodi nchini zikiwemo kuwasilisha ritani za VAT, ritani za kodi ya mapato na kutoa risiti sahihi za EFD,

**(v)** Kuwa ni kosa la kisheria kwa Consolidator au De-consolidator kugomboa na kulipia kodi mizigo ya watu wengine inayoingia nchini kwa kutumia jina la Consolidator au De-consolidator badala ya jina la mwenye mzigo.

Wafanyabiashara na Umma kwa ujumla unajulishwa juu ya kuzingatia tangazo hili ili kuisaidia TRA kutimiza wajibu wake ikiwa ni pamoja na kutunza taarifa sahihi za walipakodi nchini. Katika hatua nyingine tutafanya ukaguzi maeneo ya biashara ikiwa ni muendelezo wa ukaguzi wa kawaida kufuatilia namna wafanyabiashara wanavyoingiza mizigo yao nchini pamoja na kuhakiki nyaraka husika.

***Utekelezaji wa maagizo yaliyoko kwenye tangazo hili unaanza mara moja kwa mizigo inayoagizwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.***

***Aidha kwa wale ambao mizigo yao ipo njiani, wanapewa siku tisini (90) kuanzia tarehe ya tangazo hili wakamilishe taratibu za ugomboaji ikijumuisha ulipaji wa kodi stahiki.***

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Imetolewa na:**
**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPA KODI**
**TRA MAKAO MAKUU**

217327202

# Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Simba, Yanga hamasa ya Rais Samia izae matunda*

**RAIS** wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, amezipongeza Klabu Kongwe nchini Simba na Yanga kwa kuendelea kuchangamkia fursa aliyotoa ya Sh. milioni tano kwa kila bao zinazofunga kwenye michuano ya kimataifa, Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika.

Jana katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya kilele cha miaka miwili ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita iliyoandaliwa na Umoja wa Wanawake wa CCM Tanzania (UWT), Rais Samia alizungumzia ushiriki wa Simba kwenye Ligi ya Mabingwa na Yanga kwenye Kombe la Shirikisho, ambapo amekuwa akitoa Sh. milioni tano kwa kila goli linalofungwa na timu hizo.

Tunatambua nia hasa ya Rais Samia ni kuona dhamira yake ya sekta ya michezo kukua na kuitangaza nchi, inafanikiwa na ndiyo maana alitoa ahadi hiyo na amekuwa akiitekeleza kwa ufanisi mkubwa tena papo kwa papo kila baada ya mechi kumalizika kupitia kwa Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, iwe zimepata ushindi ndani ama nje ya nchi.

Tayari Yanga ambayo ilitarajiwa kushuka Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana usiku dhidi ya US Monastir ya Tunisia, imeshalamba Sh. milioni 30 kwa mabao sita iliyofunga hadi sasa, huku Simba ikiondoka na milioni 45 kutokana na mabao yao tisa, hivyo kwa ujumla Rais Samia ameshatoa Sh. milioni 75.

Pamoja na kiasi hicho kikubwa, lakini Rais Samia amezitaka Simba na Yanga kuendelea kuweka mpira nyavuni kwa kuwa mamilioni bado yapo ya kutosha, lengo lake likiwa ni kuona zikilitangaza soka la Tanzania na nchi kwa ujumla.

Kadhalika, dhamira kuu ya Rais Samia si kuona tu zikifunga mabao, bali anatamani kuona zikipata ushindi na mafanikio makubwa kwa kufika mbali na hatimaye kutwaa ubingwa wa michuano hiyo mikubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Nipashe hicho ndicho tunachokiamini hasa tukitambua kuna mahitaji mengi na ya muhimu zaidi ambayo Rais Samia anahitaji kuelekeza nguvu huko, lakini kwa kutambua kwamba michezo pia ni sekta nyeti na imekuwa fursa kubwa kwa kutoa ajira kwa vijana nchini, kwa makusudi kabisa ameamua kutoa hamasa huko ili kuwa kichocheo cha mafanikio.

Hivyo, ni wakati muafaka kwa wachezaji, viongozi na makocha kutendea haki mkono huu wa Mama Samia kwa kujituma zaidi ili kufika mbali zaidi na kumvutia ili kuendelea kumulika sekta ya michezo nchini.

Watanzania wana imani kubwa na anachokifanya Rais Samia hususan katika sekta ya michezo, hivyo tunataka kuona Simba na Yanga zinaitumia fursa hiyo vema ili kuwa kichocheo cha timu nyingine nchini kufanya vizuri kila zinapopata nafasi ya kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa.


Tayari Simba imefuzu hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa na Yanga ilikuwa ikihitaji tu ushindi jana usiku ili kutinga hatua hiyo kwa upande wa Kombe la Shirikisho Afrika, hivyo hamasa hii anayoendelea kuitoa Rais Samia, tunatamani kuona zikiguswa na kujituma zaidi ili kutinga nusu fainali na hatimaye fainali na kutwaa kabisa ubingwa.

Kwa uwezo zinazouonesha kwenye michuano hiyo, tunaamini hakuna kinachoshindikana kama zitaendelea kujiimarisha na kufanyia marekebisho makosa zinayoyafanya kila baada ya mechi.

Kwa hapo zilipofikia, tayari Tanzania ina nafasi ya kuingiza timu nne kwenye michuano hiyo ijayo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika kwa msimu wa 2023/24, hivyo ni fursa kwa klabu zetu zitakazofuzu kujipanga kufanya vizuri ili kwenda kukata kiu ya Rais Samia ya kuona taji hilo kwa Tanzania linaanza kuwa ni nyumbani kwake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

## *Tuwaache makocha wafanye kazi zao*

**SIDHANI** kama kuna shabiki wa Simba leo anamlalamikia Kocha Mkuu, Robertinho Oliveira, kuwa hafai na ameleta mfumo mbaya kwenye kikosi hicho.

Leo kila mmoja anashangilia timu kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa, ikiwamo kuifumua Horoya AC mabao 7-0 juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Inawezekana kabisa miongoni mwao kwa sasa ukawasaka wale waliokuwa wakimnyooshe kidole au kutokuwa na imani naye, ukawakosa, kila mmoja anakwambia si yeye aliyekuwa akisema hayo.

Robertinho hakuingia Simba kwa mguu mzuri, kwani baada ya kupewa jukumu la kukikoa kikosi kilianza kuonekana kusuasua na kupata ushindi wa tabu kiasi cha kuanza kunyooshewa vidole vya shahada na wachambuzi, ambao kwa kiasi kikubwa ndiyo walioshambuliwa hata na baadhi ya wanachama na Simba.

Wanasimba sasa wakawa wanamlinganisha na kocha aliyekuwa akikaimu, Juma Mgunda, ambaye wao waliona ndiye alifaa kuendelea kukinoa kikosi kwa sababu kilifanya vema kwenye mechi za kufuzu kutinga hatua ya makundi, kikishinda mechi zote nne za mwanzo dhidi ya Nyasa Big Bullets ya Malawi na C.D Primeiro de Agosto ya Angola.

Lakini wakashindwa kutofautisha ugumu wa mechi za mchujo na za makundi, zote zikaonekana ni sawa tu. Cha ajabu Mgunda mwenyewe bado yupo kwenye kikosi hicho hicho, lakini walivyokuwa wanaongea ni kama vile alikuwa ametimuliwa.

Leo hii Robertinho amegeuka shujaa kwani ametinga kwenye hatua hiyo akiwa na kikosi ambacho wengi hawakutegemea kama angeweza kufanya hivyo.

Kikosi hiki kilichotiliwa mashaka zaidi kuliko vyote ndicho kilichoweka rekodi ya kufunga mabao mengi zaidi kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa kwa mara ya kwanza kwenye historia ya klabu hiyo, tena dhidi ya timu kubwa, yenye viwango vya juu vya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Horoya.

Kikiwa chini ya Robertinho, kikosi hiki ambacho kinaonekana bado kina mapungufu kadhaa, lakini amekisuka kutokana na raslimali alizokuwa nazo na kuweza kukifanya ambacho wengi waliona hakiwezekani.

Mashabiki wengi na baadhi ya wachambuzi walidai kuwa Robertinho amebadilisha falsafa ya Simba ya kucheza kile kinachoitwa 'pira biriani', na kutengeneza mfumo wa kucheza soka la moja kwa moja na si lile la kupiga pasi nyingi.

Wengi wakadhani kuwa zile pasi nyingi za Simba ndiyo zilikuwa zinasababisha timu iwe inapata ushindi. Ikumbukwe kikosi cha msimu uliopita kilitolewa kwenye Ligi ya Mabingwa na kwenda Shirikisho barani Afrika, na hiki ambacho kilikatiwa tamaa kabisa kimetinga hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa.

Binafsi, tangu mwanzo sikuwa na wasiwasi wa Robertinho na nilitegemea ni suala la muda tu watu wataanza kumwelewa na kumuimba kwa mapambio ya kuvutia.

Sikuwa na wasiwasi kwa sababu haiwezekani kocha aziongoze vema timu za Rayon Sport ya Rwanda na Vipers ya Uganda akizipatia mafanikio wakiwa na wachezaji wa kawaida tu, ashindwe kwenye Klabu ya Simba yenye wachezaji wazoefu na wakubwa.

Ambacho Robertinho amekibadilisha Simba ni kutocheza pasi nyingi fupi fupi kwa taratibu huku zikiwa hazina maana yoyote zaidi ya kufurahisha mashabiki.

Ametengeneza mfumo wa kucheza soka la moja kwa moja kushambulia kwa kasi na kurejea kwa haraka wanapopoteza mpira. Awali, wachezaji wengi wa Simba na hadi sasa wengine wanashindwa kuendena na hilo kwa sababu hawajazoea. Wengine umri unawatupa mkono. Kwa sasa wanaonekana kuingia kwenye mfumo wa mwalimu taratibu, kiasi kwamba imeanza kutengeneza nafasi nyingi za kufunga, lakini tatizo kuwa lilikuwa ni umaliziaji. Na hilo linaonekana limeanza kufanyiwa kazi. Kuanzia mechi dhidi ya Vipers, Mtibwa Sugar na Horoya, timu imeonekana kutengeneza nafasi nyingi huku ule mfumo wa kocha ukianza kukubali.

Nina uhakika wanachama na mashabiki wa Simba wataanza kumfaidi Robertinho na falsafa zake msimu ujao ambapo yeye mwenyewe na viongozi wa klabu hiyo watakapokaa kuchuja baadhi ya wachezaji wa kuachwa na wale ambao atapendekeza wasajiliwe kuendana na mfumo wake. Anaweza kufanya makubwa sana na kuwashangaza wengi.

Siku zote mashabiki wanatakiwa kubaki kwenye eneo lao la msingi la kushangilia na kutoingilia mambo ya ufundi ya kocha. Tuwaache makocha wafanye kazi zao.

## PIC yabaini tatizo la miundombinu Bandari Karema

**Na Neema Hussein,** KATAVI

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), imetembelea mradi wa Bandari ya Karema Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi na kubaini changamoto ya miundombinu ikiwamo barabara na kusababisha mizigo kushindwa kuingia na kutoka.

Mwenyekiti wa PIC, Jerry Silaa, alisema mpango wa serikali wa kujenga bandari hiyo uko pamoja na ujenzi wa barabara ya kilometa 110 pamoja na reli inayoelekea katika bandari hiyo.

Alisema kikubwa ni kuendelea kuishauri serikali kuongeza kasi ya utekelezaji wa miundombinu hiyo kutokana na matumizi ya bandari kuwa chini kwa kushindwa kupitisha magari makubwa ya mizigo katika barabara hiyo.

"Kama gari ndogo tu zimeshindwa kupita basi gari kubwa haziwezi kupita pale pamoja na bandari kukamilika kwa asilimia 100 na bandari hiyo inaweza kupunguza msongamano Tunduma maana mizigo ya Congo malori yanatumia siku 45 mpaka yavuke Tunduma yaje Zambia sasa bandari inaweza kusaidia badala ya kupita Tunduma yakapita Tabora Mpanda hadi Karema inakua rahisi kufika kwenye Bandari ya Congo.

"Vilevile hapa Katavi kuna kilimo kikubwa sana cha mahindi na mpunga tumeona Waziri wa Kilimo anahitaji wakulima kuuza mazao yao nje mazao yale yatafikaje bila kuwa na bandari kwa hiyo kwa kazi hiyo niipongeze serikali ya mama Samia Suluhu Hassan kwa ujenzi wa Bandari, kikubwa nikuunganisha miundombinu nilioitaja ili bandari iweze kufanya kazi," alisema Silaa.

Baadhi ya wananchi wanaotumia barabara ya kutoka Mpanda kuelekea Karema, wameiomba serikali kutatua tatizo la barabara hiyo kwa haraka ili kuepusha usumbufu wa abiria kukwama njiani kwa saa kadhaa kutokana na magari kushindwa kupita.

"Hapa ukienda vibaya unaweza ukaharibu chombo chako au ukahatarisha maisha ya binadamu tunaomba serikali iangalie kwa jicho la upana hivi ni kutokana na mvua iliyonyesha jana je na leo ingenyesha ingekuaje?" Alihoji Donald Kwilasa.

Bandari ya Karema imegharimu zaidi ya Sh. bilioni 47, toka imefunguliwa Septemba 2022 katika hatua ya matazamio imeingiza Sh. milioni 4.8.

# Kiwanda cha 'glove' chahitaji bilioni. 12/- kukamilika

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

ZAIDI ya Shilingi bilioni 12 zinahitajika kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha mipira ya mikono (gloves) kilichoko Idofi Makambako mkoani Njombe kinachotarajia kuanza uzalishaji mwezi Julai, mwaka huu.

Mkurugenzi Mkuu wa Bohari ya Dawa (MSD), Mavere Tukai, alisema hayo wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), walipotembelea kiwanda hicho.

Alisema kiasi cha shilingi bilioni 16 zimeshatumika mpaka sasa. Pia alisema bajeti imekuwa tatizo kubwa la kukamilisha ujenzi wa kiwanda hicho hasa kufikia hatua ya mwisho.

"Cha kwanza kabisa kukamilisha, tulichofanya ni kupitia changamoto sehemu yoyote ambayo haijakamilika hasa kwenye upande wa kukidhi mahitaji ya kisheria na mahitaji mengine ya kitaalamu lazima yawapo kwa mfano TMDA wanamatakwa yao, watu wa OSHA, mazingira, ardhi na TBS kwa hiyo tumeweka sawa hilo, suala la maabara yetu kwa ajili ya vifaa tunavyozalisha kuvipima tumekamilisha na sisi mwezi Juni tutakuwa tumemaliza maandalizi yote ya kiwanda na kuanzia mwezi Julai tutaanza uzalishaji moja kwa moja," alisema.

"Kwa sasa nini kinahitajika sisi kwa upande wetu kama tulivyowasilisha kwenye kamati kwamba kuna fedha inahitajika ili kiwanda kiwe kimekamilisha kila hitaji, tutaanza uzalishaji itakuwa imekamilika, lakini bado kuna fedha tumeomba, tunaomba pia waendelee kuwa mabalozi wetu katika kuhakikisha tunapata zile fedha kutoka serikalini," alisema Tukai.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Japhet Hasunga, Mbunge wa Jimbo la Vwawa kwa niaba ya Kamati ya Bunge, amekiri kupokea maombi ya kiwanda hicho na kuahidi kwenda kuyafanyia kazi.

"Sisi kama kamati kwanza tulikuja kuangalia kama fedha ambazo zilizotolewa zimetumikaje, baada ya hapo uongozi wa bohari wameleta maombi kwamba wamekusudia kuiomba serikali Sh. bilioni 12 ili kukamilisha vitu ambavyo vimebaki ili kiwanda hiki kiweze kuzalisha zile bidhaa ambazo zinahitajika. Na sisi tuseme tumelichukua tutapitia ile taarifa halafu tuishauri serikali," alisema Hasunga.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini MSD, Rosemary Silaa, alisema licha ya kutarajia kuanza kuzalisha mipira katika kiwanda hicho, pia kitazalisha ajira hadi kwa wakulima wa zao la mpira.

"Kwa hapa Idofi tutaanza na gloves kama mlivyoona kiwanda kipo tayari, mashine zimekwishafungwa na uzalishaji wa awali kwa ajili ya kuangalia uwezo wa uzalishaji umeshaanza, lakini bado tunaangalia kwa siku za usoni tunaweza kuzalisha bidhaa nyingine za mpira kama kondomu zote hizo ni hatua, pia tunaangalia na wakulima mbalimbali ili kuhakikisha tunapata mpira hapa nchini," alisema Rosemary.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
BODI YA MFUKO WA BARABARA



Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# SALAMU ZA PONGEZI

**Bodi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Bodi ya Mfuko wa Barabara** wanaungana na Watanzania wote kukupongeza **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka miwili ya uongozi wako.

**Ndani ya Kipindi cha Miaka Miwili:**

- Umeongeza bajeti ya kugharamia matengenezo ya barabara kwa asilimia 27 kutoka Shilingi bilioni 806.7 mwaka wa fedha 2019/20 hadi Shilingi bilioni 1,027 mwaka wa fedha 2021/22.
- Umewezesha zaidi ya kilometa 50,000 za barabara za Kitaifa na Wilaya pamoja na madaraja kufanyiwa matengenezo kila mwaka.
- Umewezesha sehemu kubwa ya mtandao wa barabara kupitika wakati wote. Asilimia 90 na asilimia 60 ya barabara za Kitaifa na Wilaya, mtawalia, ziko kwenye hali nzuri na wastani.
- Umefungua barabara nyingi za vijijini kwa kutenga zaidi ya Shilingi bilioni 440 kila mwaka kugharamia maboresho ya barabara za Wilaya.
- Umewezesha zaidi ya wanawake 4,000 kupata ajira za muda kwenye kazi za matengenezo ya barabara za Wilaya.

***Kazi Iendelee***

***Bodi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Bodi ya Mfuko wa Barabara tunakutakia kila lakheri kwenye Uongozi wako mahiri na uliotukuka***

Bodi ya Mfuko wa Barabara, Makao Makuu Dodoma, 11 Barabara ya AMMAR, 41107 DODOMA MAKULU, DODOMA
Simu : +255 26 2963277-8, Nukushi: +255 26 2963279-80, Barua pepe: info@roadsfund.go.tz, Twitter: @rfb_tz,
Facebook: www.facebook.com/RFBTZ/, Instagram: @rfb_tz

# SUWASA yaokoa mil. 200/- ujenzi miradi ya maji

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida (SUWASA), imeokoa zaidi ya Sh. milioni 200 katika ujenzi wa mradi wa maji kwenye Kata ya Unyambwa Manispaa ya Singida kwa kutumia makandarasi wa ndani.

Mkurugenzi Mtendaji wa SUWASA, Sebastian Warioba, akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa mradi huo uliofanyika Kijiji cha Unyambwa, alisema mradi huo umetekelezwa kwa 'fource account' na hadi kukamilika umetumia Sh. milioni 622 na kama ungetekelezwa kwa kutumia makandarasi zingetumika Sh. milioni 869.

Warioba alisema fedha za mradi huo zilitolewa na Wizara ya Maji kupitia Mfuko wa Maji wa Taifa na utawanufaisha wakazi 6,120 wa vijiji vya kata hiyo ambao kwa muda mrefu walikuwa hawapati huduma ya majisafi na salama.

Alisema katika mradi huo vimejegwa vituo 16 vya kuchotea maji katika maeneo mbalimbali yatakayokuwa yanazalishwa ni lita 8,000 kwa saa.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, akizindua mradi huo aliwaonya wananchi kutojihusisha na vitendo vya wizi wa maji kwa kuwa unaongeza mzigo wa gharama kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida (SUWASA) na wateja wake.

Alisema ili SUWASA iendelee kutoa huduma vizuri ya maji, wananchi wahakikishe wanajenga utamaduni wa kulipa ankala za maji kila mwezi, kutunza vyanzo vya maji na kutojihusisha na wizi.

Alitaja mambo yatakayosaidia SUWASA kuwa ni kutunza vyanzo vya maji pamoja na miundombinu yote ya huduma, kutumia maji kwa uangalifu na kufuata taratibu zilizowekwa wakati wa kuomba maunganisho ya majisafi.

Meya wa Manispaa ya Singida, Yagi Kiaratu, alisema kwa muda mrefu wananchi wa kata ya Unyambwa walikuwa wakikabiliwa na kero kubwa ya maji kwa kutumia visima wakichangia na mifugo.





# TANAPA yaagizwa kuongeza 'drones' kukabili majanga ya moto

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, ameagiza watendaji waliopo chini wizara hiyo kwa kushirikiana na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), kuboresha miundombinu na kuongeza vifaa vya kukabiliana na majanga katika hifadhi ikiwamo ndege zisizo na rubani na ndege ya kuzimia moto.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki, alipokuwa Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro kushiriki sherehe za maadhimisho ya miaka 50 ya tangu kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (KINAPA).

Alisema pamoja na hilo pia wahakikishe wanaweka mfumo ya kiusalama katika maeneo yote ya hifadhi hasa wakati wa kupanda Mlima Kilimanjaro kwa uwekaji wa camera (CCTV), kwa ajili ya kudhibiti matukio ya moto yanayosababishwa na uvutaji wa sigara.

"Upatikanaji wa ndege zisizo na rubani kutasaidia kuongeza jitihada za kiusalama na kubaini matukio yanayoweza kuathiri mlima wetu wa kilimanjaro pamoja na upatikanaji wa ndege za uthibiti na upatikanaji wa taarifa za kudhibiti mambo mbali mbali ikiwamo matatizo ya moto," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya TANAPA, Jenerali Mstaafu, George Waitara, alisema licha ya uwepo wa mabadiliko ya tabianchi yaliyosababisha kushuka kwa theluji idadi ya watalii imeongezeka kutoka 12,050 mwaka 2020/2021 hadi 47,171 mwaka 2022/23.

Kamishna Mkuu wa Uhifadhi wa TANAPA, William Mwakilema, alisema Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro, imekuwa ya pili kwenye hifadhi ambazo zinaingiza kipato na wamedhamiria kuotesha miti 1,350 katika mwinuko wa Mlima Kilimanjaro.

# Mradi utatuzi migogoro nje ya mahakama waanza K'njaro

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MRADI wa majaribio wa utatuzi na usuluhishi wa migogoro ya kifamilia nje ya Mahakama na polisi unaotumia njia mbadala za utatuzi na usuluhishi wa migogoro (ADR) umeanza kutekelezwa rasmi mkoani Kilimanjaro, ukilenga kurahisisha upatikanaji wa haki kwa haraka zaidi.

Utekelezaji wa mradi huo wa mwaka mmoja unaoendeshwa na Shirika la Kilimanjaro Women Information Exchange & Community Organization (KWIECO), kwa ufadhili wa Shirika la Legal Service Facility Tanzania (LSF), ni mahususi kwa ajili ya kuelimisha jamii husika iliyokumbwa na shauri husika. Jamii hiyo watashauriwa kuhusiana na sheria zilizoko na taratibu na haki iko upande gani ili wakubaliane na kuridhiana katika kutatua migogoro unaowahusu.

Akizungumza juzi katika Manispaa ya Moshi, wakati wa uzinduzi wa mradi huo, Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Shirika la Kiraia la KWIECO, Stuart Nathaniel, alisema mradi huo ulianza Februari na utatekelezwa hadi Desemba mwaka huu utatoa picha halisi ya utekelezaji wake na utawapa mafunzo ya kutosha na kuona namna gani wamefanikiwa katika utekelezaji.

"Kwa sasa tumeanza utekelezaji wa mradi wa majaribio wa matumizi ya ADR. ADR maana yake ni Altenative Disputes Resolution, yaani utatuzi wa migogoro ya kifamilia kwa kutumia njia mbadala, ambazo siyo za kimahakama wala za kipolisi. "Kwa hiyo mradi huu tunauanza kwa kuangalia namna ambavyo utarahisisha upatikanaji wa haki kwa haraka zaidi katika namna ya kuelimisha jamii husika iliyokumbwa na shauri husika. Mashauri ambayo yataangaliwa zaidi ni mashauri ya ndoa, matunzo kwa watoto, migogoro ya ardhi na mirathi, vipigo na udhalilishaji.

Kwa mujibu wa Stuwart, mradi huo utaaanza kufanya utafiti wa awali, ambayo itaendelea kuimarisha mwongozo wao wa namna gani wanaweza wakaboresha ili kupata mafunzo yatakayowapa mbinu sahihi, ambayo inafaa kutumika kurahisisha upatikanaji au kutatua migogoro ya kifamilia.

Mratibu wa mradi huo, Lilian Mandari, alisema lengo kuu la mradi huo ni kuchangia utatuzi wa migogoro ya kifamilia kwa kutumia njia mbadala na kupunguza mashauri yanayoweza kutatuliwa kwenye jamii.

Alisema mradi huo utaimarisha maarifa kwa watoa huduma za msaada wa kisheria, kwa kutumia njia mbadala ya utatuzi wa migogoro ya kifamilia, kuongeza uelewa wa jamii kuhusu sheria na kuimarisha mfumo wa kifamilia katika utatuzi wa migogoro kwa kuzingatiwa viwango vya sheria nchini.

Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Muhusin Kirua, alieleza faida za mradi huo kuwa walengwa wa shauri husika watakaopita katika jopo la watoa huduma, baada ya usuluhishi kufanyika nje ya mahakama kuishi kwa amani na upendo, kwa sababu hakupatikana mshindi katika kesi yao.

Aliitaja faida nyingine, ni ADR inaokoa gharama kwa sababu unapofungua shauri mahakamani kuna gharama za ada ambazo zinatakiwa kulipwa lakini kwenye ADR hakuna gharama.

Alisema pia migogoro hiyo itakuwa inasuluhishwa kwa muda mfupi, tofauti na mahakama kesi inaweza ikachukua muda mrefu na faida nyingine ADR inapunguza mrundikano wa kesi mahakamani.

Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Mrakibu Asia Matauka, akizungumzia mradi huo alisema:"Katika uwezeshaji wa huu mradi wa kutatua migogoro ya kifamilia kwa njia mbadala, kwa maana ya nje ya mahakama, binafsi ninaona ni mradi mzuri na unaweza kuleta tija katika jamii."



Meneja wa Barrick nchini, Melkiory Ngido, akieleza jinsi kampuni ya Barrick inavyotekeleza sera ya ushirikishaji Watanzania waweze kunufaika na sekta ya madini wakati wa mkutano wa Jukwaa la Pili la Utekelezaji wa Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini uliomalizika mjini Arusha mwishoni mwa wiki. Barrick pia ilikuwa mdhamini mkuu wa mkutano huo ulioandaliwa na Tume ya Madini nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uholanzi yatenga bil.2.3/- ufadhili wa mafunzo vyuo vikuu

**Na Mwandishi Wetu,** ARUMERU

UHOLANZI imetenga Dola za Marekani milioni moja (Sh. bilioni 2.3), kwa ajili ya ufadhili wa mafunzo kwa vyuo vitatu nchini vilivyoko chini ya Baraza la Taifa la Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Sayansi (NACTEVET), ili kuwawezesha Watanzania kujiajiri wenyewe hususani vijana.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Franklin Rwezimula, alisema miongoni mwa vyuo vitakavyonufaika na ufadhili huo ni Chuo cha Mifugo Tengeru kilichoko mkoani Arusha.

Dk. Rwezimula aliyasema hayo wakati akizungumza na Balozi wa Uholanzi nchini Tanzania, Wiebe de Boer, aliyekwenda kushiriki ufungaji wa mradi wa kuongeza ujuzi na mafunzo ya kujenga uwezo katika sekta ya ndogo ya kilimo cha mboga.


"Huu mradi unaofunga leo (juzi), umeendeshwa kwa takribani miaka mitatu baada ya serikali ya Uholanzi kutoa ufadhili kwa vyuo vilivyopo chini ya NACTEVET. Kimsingi mradi huu umeboresha mitaala kuendana na wakati uliopo, kwa maana ya wanaomaliza mafunzo wanakuwa na uwezo wa kujiajiri wenyewe.

Aidha, Katibu Mkuu huyo, alisisitiza kuwa mradi huo ulilenga zaidi kilimo cha matunda na mboga kwa vitendo zaidi, tofauti na dhana ya kukaa darasani kujifunza kwa nadharia.

Alivitaja vyuo vilivyonufaika na mradi huo kuwa ni pamoja na Chuo cha Mifugo Tengeru (TARI), MATI-Uyole na Chuo cha Mahinya kilichoko Wilaya ya Songea, mkoani Ruvuma, ambavyo mbali na kupata mafunzo, pia vilijengewa Green House (jumba kitalu) ili kuboresha mazao ya bustani na kuyaongeza mnyororo wa thamani mazao hayo.

Mwakilishi wa Katibu Mtendaji Baraza la Taifa la Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Ufundi Stadi, Dk. Amani Makota, alisema mafunzo hayo yameviinua vyuo hivyo kwa kuwapatiwa vifaa vya kufundishia kwa vitendo tofauti na ilivyokuwa awali wakitumia zaidi nadharia na badala ya vitendo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Balozi wa Uholanzi nchini, Wiebe de Boer, alisema wanatambua umuhimu wa ushirikiano kati ya Tanzania na Uholanzi, hivyo kwa kutambua umuhimu wa mazao ya bustani waliona ni vyema kutoa ufadhili huo.



# Kamati ya Bunge yatoa hadhari uharibifu vyanzo vya maji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KAMATI ya Bunge ya Kudumu ya Maji na Mazingira imewatahadharishwa wafugaji kuhusu uharibifu wa vyanzo vya maji kupitia shughuli za ufugaji zinazofanyika karibu na vyanzo hivyo.

Wajumbe wa kamati hiyo walitoa angalizo hilo walipofanya ziara ya ukaguzi wa mradi wa maji wa Ziwa Victoria wa Tinde-Shelui uliojengwa katika Kijiji cha Buchama, Kata ya Tinde Halmashauri ya Shinyanga Vijijini.

Mjumbe wa kamati hiyo, Mhandisi Stella Manyanya, alisema uharibifu huo umekuwa ukifanyika mara kadhaa, wakati wakitafuta maji ya kunyweshea mifugo yao wakiwa marishoni, hali ambayo inasababisha serikali kutumia gharama kubwa kuikarabati.

Alisema kuna haja ya kutoa elimu kwa wafugaji ikiwa ni pamoja na kushirikiana katika ujenzi wa bauti ya kunyweshea mifugo yao wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo ili kuepuka uharibifu unaozidi kuingizia serikali hasara.

Emmanuel Cherehani ambaye ni mjumbe wa kamati hiyo alisema kila kijiji ambacho kinapitiwa na bomba la maji wafugaji wa eneo hilo wajengewe bauti za kunyeshea mifugo yao. Diwani wa Tinde, Japhati Makwaya, alisema wananchi wanalaumu mara kwa mara kuwapo kwa miradi mikubwa inayopitisha maji katika maeneo yao, huku wao hawana huduma hiyo ya maji. Makwaya alisema wakati vijiji vya pembezoni vikipata majisafi na salama wao wanaopitiwa na bomba pamoja na tangi kubwa la maji hawapati huduma hiyo, hivyo kuiomba serikali miradi itapokamilika vijiji vilivyoko jirani vipewe kipaumbele kupata huduma.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Nadhifa Kemikimba, alisema watashirikiana na Wizara ya Mifugo katika kujenga bauti za kunyweshea mifugo sehemu bomba la maji litakapopita ili kuondoa uharibifu huo.

Alisema bauti moja inagharimu zaidi ya Sh. milioni 10 hadi kukamilika kwake, huku akiwatahadharisha wafugaji kuwa makini na miundombinu hiyo.

Alisema kila mmoja anawajibu wa kutunza vyanzo vya maji pamoja na miundombinu yake ili kuhakikisha inawanufaisha watu wote licha ya kuwa na kamati maalumu za utunzaji na uangalizi wa vyanzo.



Waajiri wa Sekta Binafsi mkoani Shinyanga wakiwa kwenye Semina ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwa ajili ya kukumbushwa majukumu yao na wajibu wao kwa kupeleka michango ya akiba ya fedha za mafao kwa watumishi wao, juzi **PICHA: MARCO MADUHU**

# SBL yatoa ajira kwa wakulima 200,000

**Na Titus Mwombeki,** BUKOBA

WAKULIMA wapatao 200,000 kutoka maeneo mbalimbali nchini wamenufaika na shughuli za kilimo pamoja na kupata ajira kutoka Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), ambayo kila mwaka huchangia kodi ya Sh. bilioni mbili.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi Mkuu wa SBL anayemaliza muda wake, Mark Ocitti na kusema kuwa lengo ni kumwinua mkulima pamoja na vijana.

Alisema kampuni hiyo inapanga kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka nchi zenye uhitaji wanaosomea stashahada ya kilimo chini ya mpango wake wa ufadhili unaoitwa 'kilimo viwanda' ambao umewanufaisha zaidi ya wanafunzi 230 katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema serikali inatambua mchango wa wawekezaji nchini katika kuhakikisha sekta ya viwanda nchini inakua na kuongeza pato la Taifa.

"Kwa miaka mitatu iliyopita Ocitti amekuwa pamoja nasi hapa nchini, amedhihirisha kuwa yeye ni kiongozi mwenye maono, ambaye alitaka kuipeleka SBL juu zaidi, na hii siyo kwa SBL tu kama kampuni ila pamoja na wafanyakazi wa SBL na taifa kwa ujumla." Alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya SBL, John Ulanga, alitoa shukrani kwa Ocitti kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi wa SBL, akibainisha mafanikio ya Ocitti katika miaka mitatu ya uongozi wake.

Katika hafla ya kumuaga, SBL ilimtambulisha Mkurugenzi Mtendaji wake mpya, Obinna Anyalebechi ambaye anajiunga na biashara hiyo kutoka Uingereza.

# Wanafunzi waiangukia serikali kujengewa vyoo

**Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari Sengerema iliyopo wilayani Sengerema mkoani Mwanza wameiomba serikali pamoja na wadau wa elimu kuwajengea matundu ya vyoo shuleni hapo.

Wakizungumza na waandishi wa habari kwa nyakati tofauti, wanafunzi hao wa kidato cha sita walisema idadi yao wapo 80 na kwamba wanatumia tundu moja la choo kwa zamu.

"Tunaomba serikali kwa kushirikiana na wadau wa elimu wajitahidi kuboresha miundombinu ya choo ili kuondoa adha ya kusubiriana muda mrefu tukihitaji huduma ya choo," alisema Amos John.

Kadhalika wanafunzi hao walisema wamekuwa wakipata tatizo la usafiri pindi mwanafunzi anapougua ghafla hasa nyakati za usiku, wanashindwa kumpeleka hospitali kwa wakati kutokana na ukosefu wa gari la wagonjwa shuleni hapo.

Akieleza juu ya adha hizo zinazowakumba wanafunzi, Mkuu wa shule hiyo, Zacharia Kahema, alisema tayari amechukua hatua ya kufikisha tatizo hilo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri.

Ofisa Elimu wa Shule za Sekondari katika Halmashauri ya Sengerema, Genoviva Chuchuba, aliahidi kulifikisha tatizo hilo katika mabaraza ya halmashauri ili kuweza kutengewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyoo.

Shule hiyo ina wanafunzi 1,309, wanaotarajiwa kufanya mtihani wa kidato cha sita mwaka huu ni 678.

Nipashe
# Spotika



'WAFUNGAJI WA5 BORA WA MUDA WOTE EPL' UKURASA 14




# 'VINYOZI' BORA WA WAKATI WOTE UEFA

**LONDON,** England

HUKU Ligi ya Mabingwa Ulaya ikiandaa baadhi ya timu na wachezaji wakubwa tangu mwaka 1992, rekodi zinavunjwa kila mwaka.

Kilele cha soka kwa klabu kinachotawala hatua kubwa zaidi ya Ulaya ni moja ya sehemu ya mafanikio makubwa zaidi kwa klabu.

Makala haya inawaangalia wafungaji bora wa muda wote wa mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Wachezaji hawa waling'ara wakati wakiwa na timu zao na kuziwezesha kutwaa taji hilo ambalo ni kubwa zaidi kwa ngazi ya klabu barani Ulaya.

**#5. Raul (Mabao 71)**

Gwiji wa Real Madrid na Raul alikaa vema kileleni mwa jedwali la wafungaji akiwa na mabao 71 alipostaafu.

Lakini katika miaka ya hivi karibuni Mhispania huyo ameangushwa hadi nafasi ya tano kwenye orodha hiyo na Mfaransa na nyota wa 'Los Blancos' hao, Karim Benzema.

Raul alikuwa na maisha ya hali ya juu, akishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu akiwa na klabu yake ya nyumbani na kutajwa kuwa mfungaji bora wa mashindano hayo mara mbili.

**#4. Karim Benzema (Mabao 89)**

Benzema ndiye mfungaji bora wa nne katika mashindano haya ya soka ya klabu barani Ulaya na bao jingine katika ushindi wa mkondo wa pili dhidi ya Liverpool limemfanya asonge mbele zaidi ya tatu bora.

Sasa ana umri wa miaka 35, Mfaransa huyo aliifungia Lyon katika mechi yake ya kwanza ya michuano hiyo akiwa na umri wa miaka 17 pekee.

Mabao yake yameisaidia Real Madrid kutawazwa mabingwa wa Ulaya mara tano wakati wake pale Bernabeu. Na Benzema huenda akastaafu soka akiwa kwenye orodha ya juu kwa ufungaji kwenye mashindano hayo.

**#3. Robert Lewandowski (Mabao 91)**

Nyota wa zamani wa Bayern Munich, Robert Lewandowski alifikisha alama 80 katika muda wa rekodi baada ya kuchukua mechi 100 pekee - mbili pungufu kuliko mchezaji aliyefuata kwenye orodha hii.

Mabao 15 ya raia huyo wa Poland katika msimu wa 2019-2020 yalimfanya achukue Kiatu cha Dhahabu na kuiongoza timu yake kutwaa ubingwa.

Lakini hatakuwa na nafasi ya kufunga tena msimu huu kwani Barcelona ambayo anaichezea kwa sasa haipo kwenye mashindano hayo.

**#2. Lionel Messi (Mabao 129)**

Mchezaji nyota wa Argentina, Lionel Messi ametamba Ligi ya Mabingwa Ulaya mara nyingi tangu mwaka 2005 na ni wa tatu katika orodha ya wachezaji waliocheza muda wote.

Akitumia sehemu kubwa ya maisha yake ya soka kuichezea timu yake ya utotoni ya Barcelona, amefunga mabao ya kutosha na kunyanyua kombe hilo maarufu mara nne.

Na ameendeleza uchezaji wake kule Paris Saint-Germain, lakini bado hajaweza kuisaidia timu hiyo ya Ufaransa kupata mafanikio kwenye mashindano hayo.

**#1. Cristiano Ronaldo (Mabao 140)**

Cristiano Ronaldo ni mashine ya kufunga mabao bila ubishi. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno ametikisa nyavu mara 140 kwa klabu tatu, huku nyingi zikipatikana wakati akiwa Real Madrid.

Ronaldo amecheza mechi 183 kwenye michuano hiyo tangu alipoanza kuichezea Manchester United mwaka 2003.

Akiwa na mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya chini ya Madrid na moja kutoka kwa Mashetani Wekundu, mshambuliaji huyo ni mmoja wa wachezaji bora zaidi waliopambwa zaidi kuwahi kutokea.

Nyota wa zamani wa Juventus, Ronaldo mwenye umri wa miaka 38, pia ndiye mchezaji wa kwanza kufunga katika fainali mbili kwa timu mbili tofauti zilizoshinda - akifunga bao la kwanza kwa United mwaka 2008 na penalti ya dakika ya 120 kwa Real mnamo 2014.

## ISIKUPITE

Clatous Chama (Simba - Tanzania) na Makabi Lilepo (Al Hilal - Sudan) hadi kufikia raundi hii ya tano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ndio wanaoongoza kwa ufungaji wa mabao kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, kila mmoja akicheka na nyavu mara nne, wakifuatiwa na Cassius Mailula (Mamelodi Sundowns - Sauzi), Mahmoud Kahraba (Al Ahly - Misri) na Peter Shalulile (Mamelodi Sundowns), ambao kila mmoja amefumania nyavu mara tatu.



## Extra Time


Mshambuliaji wa Simba, Jean Baleke (kushoto), akishangilia na wenzake, Saido Ntibazonkiza, Mohamed Hussein 'Tshabalala' na Shomari Kapombe, baada ya kuifungia timu yake bao la pili wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 7-0 dhidi ya Horoya AC ya Guinea, kwenye mechi ya Kundi C ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# REKODI 5 ZAKUVUTIA SIMBA IKITINGA ROBO FAINALI CAF

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya nne, timu ya Simba imefanikiwa kuingia hatua ya robo fainali ya michuano ya kimataifa kwa kipindi cha miaka mitano.

Juzi imefanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ilipoirarua bila huruma, Horoya AC ya Guinea mabao 7-0 mechi ikipigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ushindi huo unaifanya timu hiyo kutinga hatua ya robo fainali Ligi ya Mabingwa kwa mara ya tatu na mara moja Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Kwa kipindi chote hiki, Simba ilikuwa inatinga vipi kwenye hatua hiyo? Makala haya yanakuletea hatua zote ambazo timu hiyo ilikuwa inatinga, huku baadhi ya wachezaji wakiweka rekodi mbalimbali.

**Mara tatu robo Ligi ya Mabingwa**

Mara ya kwanza Simba kutinga hatua hiyo ilikuwa ni Machi 16, mwaka 2019, ilipoifunga AS Vita Club ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa yaliyofungwa na Mohamed Hussein 'Tshabalala' na Clatous Chama, huku wageni wakianza kutangulia kwa bao la Kazadi Kasengu ambaye kwa sasa yupo Singida Big Stars.

Simba ilikuwa Kundi D, ikasonga mbele kwa pointi tisa, ikifungwa mabao 5-0 mara mbili na timu za Al Ahly ya Misri na AS Vita Club ikiwa ugenini, na mabao 2-0 dhidi ya JS Saoura ya Algeria, lakini ikapiga hesabu zake vema kama kawaida kwenye uwanja wa nyumbani, ikaichapa JS Saoura mabao 3-0, Al Ahly ikafa bao 1-0, kabla ya kutinga hatua hiyo kwenye mechi dhidi ya AS Vita.

Msimu wa 2020/21, Simba ilirudia tena ilichokifanya 2019, ilipofanikiwa kutinga robo fainali hapo hapo kwa Mpaka, ikiifunga tena timu hiyo hiyo ya AS Vita Club, Aprili 3, 2021, lakini safari hii mabao 4-1.

Safari hii tena, Simba ilipangwa kundi moja na Al Ahly pamoja na AS Vita Club, kilichobadilika ni timu moja, badala ya JS Saoura, ikaingia Al Merrikh ya Sudan, pia idadi ya mabao, kwani Wakongo walikufa mabao 4-1 kwa Mkapa.

Yalikuwa ni mabao mawili ya Chama dakika ya 45 na 84, Luis Miquissone na Rally Bwalya dakika ya 66 yaliyoipeleka hatua hiyo.

Ikikwa kwenye Kundi A, Simba safari hii haikuwa ya pili, badala yake ililiongoza kundi ikiwa na pointi 13, Al Ahly ambayo ilikwenda kutwaa ubingwa, ilikuwa chini yake ikikusanya pointi 10.

Simba ilishinda ugenini bao 1-0 dhidi ya AS Vita Club, ikaichapa Al Ahly bao 1-0 nyumbani, suluhu ya ugenini dhidi ya Al Merrikh, ikawachapa Wasudan hao mabao 3-0 nyumbani, ikapoteza bao 1-0 nchini Misri dhidi ya Al Ahly, kabla ya kuifanya tena ngazi As Vita Club kwa mara nyingine.

Juzi ilikuwa ni mara ya tatu, ilipata ushindi mnono wa mabao 7-0, yaliyofungwa na kiungo mshambuliaji wa timu hiyo Mzambia Clatous Chama ndiye aliyeongoza mauaji ya jana, akifunga mabao matatu 'hat-trick', straika raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Jean Balake na Saido Kanoute raia wa Mali wakifunga mabao mawili kila mmoja.

Imefikisha pointi tisa ambazo hazitofikiwa na Horoya wala Vipers, hivyo kutoka Kundi C msimu huu, imekwenda Simba na Raja Casablanca ya Morocco.

**Mara moja Kombe la Shirikisho**

Msimu wa 2020/21, Simba ilitolewa kwenye Ligi ya Mabingwa kwa namna iliyowashangaza wengi na timu dhaifu ya Jwaneng Galaxy ya Botswana, ikaangukia kwenye Kombe la Shirikisho ambako nako ilifanikiwa pia kufika hatua ya robo fainali.

Ikiwa Kundi D, ilifanikiwa kushika nafasi ya pili chini ya RS Berkane ambayo ilikwenda kutwaa kombe hilo, zote zikimaliza na pointi 10.

Mechi iliyoipeleka Simba hatua hiyo ilichezwa Aprili 3, 2022 Uwanja wa Benjamin Mkapa iliivurumisha US Gerndamerie ya Niger mabao 4-0, yaliyowekwa wavuni na Chris Mugalu aliyefunga mawili dakika ya 68 na 78, Sadio Kanoute dakika ya 63, na moja wakijifunga wenyewe.

**Mabao mengi mechi moja**

Mpaka sasa Simba imeweka rekodi ya kuwa timu iliyofunga mabao mengi kwenye mechi moja, katika hatua ya makundi ya michuano hiyo kwa msimu huu.

Kabla ya mechi ya juzi, ni mechi mbili ambazo zilikuwa na ushindi mkubwa kwa timu, kwenye kundi hilo hilo, Raja Casablanca ya Morocco iliifunga Vipers ya Uganda mabao 5-0 na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini iliiadhibu Al Ahly mabao 5-2 kwenye Kundi B.

**Chama mfalme wa robo fainali**

Kiungo Mzambia, Clatous Chama, ameweka rekodi ya kufunga mechi zote ambazo Simba ilikuwa inahitaji ushindi kwenda robo fainali ya Ligi ya Mabingwa na kufanikiwa kuivusha.

Machi 16 mwaka 2019, ilipoifunga AS Vita Club ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo mabao 2-1 alifunga bao la pili dakika ya 90, 2021 ilipoifunga AS Vita Club 4-1, akifunga mabao mawili na juzi alifunga 'hat-trick', mechi ambazo zote ilifanikiwa kupita hatua za makundi.

Chama pia anafunga 'hat-trick' ya pili kwenye mechi za hatua ya makundi, nyingine ikiwekwa na Mahmoud Kahraba wa Al Ahly, Machi 17, mwaka huu akiipa ushindi wa mabao 4-0 timu yake dhidi ya Coton Sport ya Cameroon.

**Kanoute naye wamo**

Si mara nyingi kuona Kanoute akifunga mabao, lakini mchezaji huyo raia wa Mali ameweka rekodi ya kuwa mmoja wa wafungaji wa mabao yaliyoipeleka Simba robo fainali kwenye mechi za kimataifa mara mbili.

Wakati Chama akiweka rekodi hiyo mara tatu kwenye mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika tu, Kanoute amefanya hivyo juzi na mechi za Kombe la Shirikisho barani Afrika msimu uliopita.

Aprili 3, 2022 dhidi ya US Gerndamerie ya Niger mabao 4-0, alifunga bao moja, likiwa ni moja ya mabao yaliyoiwezesha Simba kwenda robo fainali na juzi alifunga mawili.

Kwa matokeo hayo, sasa Simba inasubiri kukamilisha tu ratiba ya michuano hiyo hatua ya makundi kwa kucheza mechi ya mwisho ugenini dhidi ya Raja Casablaca ya Morocco Machi 31, mwaka huu, kwani timu hizo tayari zimefuzu.

Katika Kundi C, Horoya AC na Vipers ambazo zitakutana mechi yao ya mwisho ya hatua ya makundi, hakuna inayoweza kufikia pointi tisa ilizonazo Simba lakini pia Wekundu wa Msimbazi hao hata kama wataifunga Raja Casablanca Machi 31, hawawezi kufikisha alama 13 walizonazo Wamorocco hao.

Kwa mantiki hiyo, Raja Casablanca inatinga robo fainali ikiwa kinara wa Kundi C, wakati Simba ikienda ikiwa nafasi ya pili.

## Nukuu


"Wana miaka mingi bila kushinda Ligi ya England na hiyo inakupa ziada kidogo kushinda mechi katika dakika ya 93, 96, 98. Hicho ni kitu ambacho hatuna kwa sababu tumeshinda mfululizo," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, akieleza kusubiri kwa muda mrefu kwa Arsenal kutwaa taji la Ligi ya England kutawala ubingwa msimu huu.**



"Tulizungumza mengi kuhusu soka, tulifikiria kuhusu mechi kwa njia ile ile: Tulipenda kuwaburudisha mashabiki. Hapo zamani, tulicheza kwenye viwanja ambavyo vilikuwa katika hali mbaya na ilituzuia sote, hata Diego, lakini bado alikuwa jambo la kawaida. Kama angekuwa anacheza leo na vifaa vya kisasa na viwanja, kusingekuwa na mjadala kuhusu mchezaji bora zaidi kuwahi kutokea," **Kiungo wa zamani wa Real Madrid, Bernd Schuster, akiamini kuwa Diego Maradona angecheza kwa sasa angekuwa bora zaidi ya Lionel Messi wa PSG.**



"Mpira ni maisha yetu, ukipoteza mchezo, bila shaka huna maisha rahisi, nafikiri kila mtu nyumbani, haswa mpenzi wangu, amekuwa na wiki ngumu pia wiki na miezi iliyopita. furaha sasa tena na mimi pia. Ikiwa una siku mbaya kazini ... wewe ... sitasema neno sasa lakini haujisikii vizuri. Soka ni mchezo ambao tuna shinikizo kubwa kwenye mabega yetu. Tunataka kuwafurahisha mashabiki na usipowafurahisha basi huna wakati mzuri. Kushinda siku zote ni bora, tulishinda tena ili tufurahie siku kadhaa," **mshambuliaji wa Chelsea, Kai Havertz, akielezea presha wanayopata wachezaji baada ya ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Borussia Dortmund.**





KANE

# ‘WAFUNGAJI WA5 BORA WA MUDA WOTE EPL

**LONDON,** ENGLAND

HARRY Kane ndiye mshambuliaji pekee anayecheza nafasi kubwa katika wafungaji (vinyozi) watano bora wa Ligi Kuu England maarufu kama EPL wa wakati wote.

Muuaji huyo wa Tottenham Hotspur amekuwa akihatarisha safu ya ulinzi ya timu pinzani tangu msimu wake mzuri wa 2014-15.

Lakini licha ya kudumisha kiwango cha kustaajabisha na kushinda Kiatu cha Dhahabu kwa ufungaji bora, bado ana njia ya kwenda kumwangusha kiongozi wa sasa katika viwango vya ubora, Alan Shearer.

Makala haya inawaangalia wachezaji watano ambao ni wafugaji bora wa wakati wote kwenye Ligi Kuu England.

**#5. Sergio Aguero (Mabao 184)**

Sergio Aguero atakuwa gwiji katika Klabu ya Manchester City baada ya kufunga moja ya mabao ya kipekee katika historia ya soka ya England dhidi ya QPR na kutwaa taji la Ligi Kuu mwaka 2012.

Kabla ya kuelekea Barcelona, ambako ugonjwa wa moyo kwa bahati mbaya ulimlazimu kustaafu mapema, Aguero aliweza kufunga mabao 184 katika mechi 275 pekee za Ligi Kuu England.

Muargentina huyo alishinda mataji matano ya ligi wakati alipokuwa Etihad na kuwa mfungaji bora wa muda wote wa Man City.

Fowadi huyo anashikilia rekodi ya Ligi Kuu England kwa hat-trick nyingi zaidi, akiwa amefunga mara 12, na ndiye mchezaji pekee wa kigeni nje ya England kwenye orodha hii.

**#4. Andy Cole (Mabao 187)**

Andy Cole hakuwa mgeni kwa kuzifumania nyavu kwenye Ligi Kuu England na alikuwa mwiba mkali kwa timu alizokutana nazo.

Kwa kweli, mshambuliaji huyu wa zamani wa Manchester United na Newcastle United alikuwa mfungaji mzuri na mpiga penalti mzuri zaidi.

Cole alifunga mabao 187 katika mechi 414 za Ligi Kuu huku akishinda mataji matano katika misimu yake nane akiwa na ‘Mashetani Wekundu’ hao.

**#3. Harry Kane (Mabao 203)**

Kane amekuwa kitovu cha safu ya ushambuliaji ya Tottenham Hotspur kwa zaidi ya miaka 10 iliyopita na amefunga angalau mabao 15 katika kila misimu tisa iliyopita.

Lakini licha ya uchezaji wake kwenye eneo la hatari, hajaweza kubeba taji lolote akiwa na Spurs na anahusishwa na kuondoka. Pia mfungaji bora wa pamoja wa nchi yake akiwa na mabao 53, namba 10 wa uhakika kwa timu ya taifa na klabu yake na anaweza kupanda kwenye orodha hii kwani bado anacheza na yupo kwenye kiwango bora kabisa.

**#2. Wayne Rooney (Mabao 208)**

Wayne Rooney alimpita gwiji Bobby Charlton kama mfungaji bora wa muda wote wa Manchester United na England, ingawa Kane yuko mbali na kumpita kwa upande wa timu ya taifa, maarufu Simba Watatu.

Katika mechi 491, gwiji huyo wa Old Trafford alifunga mabao 208 na kutoa pasi za mabao 103 kwa Everton na Mashetani Wekundu.

Bingwa mara tano wa Ligi Kuu, Rooney alifurahia maisha mazuri lakini amepungukiwa kwa kiasi fulani na mfungaji bora kwenye orodha hii.

**#1. Alan Shearer (Mabao 260)**

Huwezi kutaja wafungaji mabao wa Ligi Kuu England bila kumtaja Shearer mkubwa.

Akiwa amefunga mabao 52 zaidi kwa jina linalofuata kwenye orodha, rekodi ya mshambuliaji huyo wa England itazidi kiwango.

Kufunga mara 260 katika michezo 441 kwa misimu 14 akiwa na Blackburn na Newcastle, ni kiwango cha ajabu kwa mchezaji huyo aliyekuwa akivaa jezi namba 9 na alishinda taji moja tu na tuzo nne za Mchezaji Bora wa Mwezi.

Shearer ndiye mchezaji mwenye kasi zaidi kugonga karne moja kwenye Ligi Kuu - akichukua michezo 124 pekee na anasalia kuwa mchezaji pekee kufunga zaidi ya mabao 30 katika mismu kadhaa kwenye Ligi Kuu.

## JE, WAJUA?



USHINDI wa mabao 7-0, Simba iliyoupata kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi dhidi ya Horoya AC ya Guinea juzi, unaifanya kushika nafasi ya pili katika michuano hiyo na hatua hiyo kwa kutoa kichapo kikubwa zaidi kwenye historia ya michuano hiyo, ikiwa sambamba na ASEC Mimosas iliyopata ushindi kama huo mwaka 2001 dhidi ya CR Belouizdad, nafasi ya kwanza ikiongoza TP Mazembe ambayo mwaka 2019 ilishinda 8-0 dhidi ya Club Africain na nafasi ya tatu inashikwa na Raja Casablanca iliyoichapa Yanga 6-0 mwaka 1998.



# W'biashara sokoni watakiwa kuacha kukwepa kodi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAFANYABIASHARA katika masoko ya Jiji la Dodoma wameshauriwa kuacha kukwepa kulipa kodi ya mapato ili kufanikisha serikali kuwaletea maendeleo.

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Soko la Bonanza linalouza samaki wabichi, mboga na matunda, Goha Magwai, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wa uchaguzi wa soko hilo.

Aliwataka wafanyabiashara hao kuunga mkono serikali kwa kutoa kodi ya mapato badala ya kukwepa jukumu hilo ambalo ni muhimu kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania.

"Hakuna maana yoyote ya kukwepa jukumu la kutoa kodi ya mapato wao kama wafanyabiashara, kinachotakiwa ni kungana na serikali kwa uaminifu ili mapato hayo yapatikane kwa ajili ya kuleta maendeleo kwa Watanzania,"alisema.

Mwenyekiti huyo ambaye amechaguliwa kuliongoza soko hilo kwa kipindi cha miaka mitatu, alisema kuwa soko hilo pia litaanzisha mfumo wa kanzi data kwa kufanya usajili kwa wafanyabiashara wote ili kupata takwimu sahihi ya wafanyabiashara.

Alisema kuwa usajili huo ni pamoja na kuwapatia vitambulisho maalum, kwa ajili ya kuwatambua wao wenyewe na meza zao ambazo pia zitakuwa na namba.

Aidha, alisema soko hilo litahakikisha linaondoa watoto walio chini ya miaka 18 sokoni hapo wanaojishughulisha na ubebaji wa mizigo ya wateja.

Pia alisema kwa wabeba mizigo ambao waliozidi umri wa miaka 18 watafanyiwa usajili na kuwapatia sare yenye namba.

"Kwa sasa Dodoma ni Jiji na hili Soko la Bonanza siyo soko kwa ajili ya wakazi wa Dodoma tu bali ni soko la kitaifa na ndilo soko maalumu kwa kuuza matunda na mboga, samaki wabichi na miwa, hivyo tunapokea watu mbalimbali ambao wanaingia sokoni kwa ajili ya kununua mahitaji,"alisema.

Katibu wa soko hilo, Eliana Kaboyoka, alisema atahakikisha anawaunganisha wafanyabiashara wanafanya kazi kwa umoja na mshikamano sambamba na kufanya kwa ukaribu na viongozi wa serikali.

Alisema atahakikisha viongozi wanakuwa wabunifu wa vyanzo vipya vya mapato kwa ajili ya kuwainua wafanyabiashara.

# Kampuni kuzalisha tani milioni moja ya saruji Kongwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAMPUNI ya Libyan Petrolian kutoka Libya imeingia makubaliano ya awali na Kampuni ya Alotab and Black BB ya hapa nchini kwa ajili ya kuwekeza kiwanda cha kuzalisha saruji wilayani Kongwa.

Kiwanda hicho kinachotarajia kujengwa katika Kijiji cha Sejeli kilichoko wilayani Kongwa mkoani Dodoma na kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani zaidi ya milioni moja kwa mwaka.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki wakati wa hafla ya utiaji saini makubaliano hayo ya awali, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema uwekezaji wa kiwanda hicho utasaidia kuinua uchumi wa wakazi wa Dodoma hususani waliopo Kongwa.

Alisema wawekezaji hao wamekabidhiwa eneo la hekari 100 ambapo kati ya hizo hekari 30 zitakuwa kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda, lakini hekari 70 zitabakia kwa ajili ya uboreshaji wa mazingira ya eneo hilo ambalo ujenzi huo utafanyika.

"Niwapongeze sana watu wa Kongwa hususani viongozi mmeonyesha ushirikiano mkubwa kuhakikisha mnawavutia wawekezaji,"alisema Senyamule.

Alisema halmashauri nyingine mnapaswa kuiga mfano wa Kongwa ambao wameangalia namna ya kuinua fursa za wananchi wa eneo hilo kwa sababu kiwanda hicho kikikamilika kitatoa fursa za ajira kwa wakazi wa maeneo hayo.

Mwenyekiti wa Libyan Petrolian and Shakf Amjed Rajab, alisema kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani zaidi ya milioni moja kwa mwaka lakini uzalishaji utaendelea kuongezeka kila mwaka.

Rajab alisema wanafurahi kupata eneo hilo la uwekezaji na wanaamini watashirikiana vizuri na serikali pamoja na wakazi wa Kongwa ili kuhakikisha kiwanda hicho kinafikia malengo.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Alotab and Black, Abdul Ally, alisema wameona eneo hilo lina fursa za uwekezaji, ndiyo maana wameomba ardhi kwa ajili ya kuwekeza kiwanda cha saruji ili kusaidia kukuza uchumi wa nchi.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kongwa, Dk. Omary Nkullo, aliwashukuru wawekezaji hao kwa kukubali kuwekeza kiwanda hicho utakaosaidia kuinua uchumi wa kazi wa Kongwa.

Aidha, alitoa wito kwa wawekezaji wengine wajitokeze kwa wingi kuja kuwekeza mkoani hapo, hususani Kongwa.



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, akizindua mradi wa maji jana katika Kata ya Unyambwa Manispaa ya Singida ambao umegharimu zaidi ya Sh. mililoni 622 na utawanufaisha wananchi 6,120 wa vijiji vya kata hiyo. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# AAFP yazindua ratiba ya mikutano, kupigia debe Katiba

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

CHAMA cha siasa cha AAFP kimezindua rasmi ratiba za mikutano ya hadhara, huku kikishauri yafanyike marekebisho yatakayoendana na hali ya sasa kwenye Katiba pendekezwa badala ya kuanzisha upya mchakato huo.

Katika uzinduzi huo uliofanyika kitaifa katika viwanja vya Chaduru B Kata ya Makole jijini Dodoma, Katibu Mkuu wa chama hicho, Rashidi Rai, alisema kinachotakiwa kwa sasa siyo kuanzisha mchakato wa katiba mpya bali ni kuukwamua mchakato wa Katiba pendekezwa kwa kufanya maboresho yatakayoendana na hali ya sasa. Rai alisema kuwa haiwezekani kwa sasa maisha ya Watanzania yalivyo magumu badala ya kuwekeza katika masuala ya afya, elimu na upatikanaji wa chakula kwa wananchi kutumia mabilioni ya fedha kwa kuanzisha mchakato mpya wa Katiba. Katibu huyo alisema hawawezi kupoteza nguvu kubwa ambazo zimetumika katika mchakato mwingine wa Katiba mpya wakati Katiba pendekezwa iliyozingatia maoni ya wananchi ipo. Awali, alisema chama hicho kimeamua kufanya mikutano ya kisiasa majukwaani kwa kuwapa nafasi wananchi kukijua chama hicho. "Sisi ni kati ya vyama vya siasa ambao tulikuwa kifungoni kwa miaka sita, lakini kwa sasa tumepata nafasi ya kufanya mikutano ya kisiasa na leo tumezindua rasmi mikutano ya hadhara na kauli mbiu yetu ni 'Siasa na maisha ya watu kwa mujibu wa Katiba ya nchi ya mwaka 1977',"alisema.

Alisema hawatafanya mikutano ya kutangaza sera za chama bali watafanya siasa ambazo zinalenga kuibua hoja za watu ambazo zilikuwa zikiwatesa zaidi ya miaka sita kwa kipindi cha kukosa mikutano ya hadhara.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE**

# MAFANIKIO YA MIAKA MIWILI YA AWAMU YA SITA YA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**1. Utangulizi**

Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Namba 06 ya Mwaka 2005. Sheria hiyo ilianza kutumika rasmi tarehe 01 Oktoba, 2005. Chimbuko la Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ni Chuo cha Kivukoni ambacho kilianzishwa rasmi tarehe 29 Julai 1961. Uamuzi wa kuanzisha Chuo hiki ulikuwa ni uamuzi wa Mkutano Mkuu wa Chama cha TANU wa Tabora 1958. Aidha, Hayati Mwalimu Nyerere, ndiye aliyekuwa muanzilishi wa Chuo hiki, wakati huo kikiitwa Chuo cha Kivukoni. Chuo kina Kampasi tatu: Kampasi ya Kivukoni iliyopo Kivukoni-Dar es salaam; Kampasi ya Karume ilyopo Unguja-Zanzibar na Kampasi ya Pemba iliyopo wilaya Chakechake Pemba.

**2. Dira**

Dira ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ni kuwa kitovu cha utoaji wa maarifa bora, elimu na mafunzo kuhusu ubunifu na uvumbuzi na kuendeleza amani na umoja wa kitaifa.

**3. Majukumu ya Chuo**

Katika kuhakikisha kuwa Chuo kinafikia Dira iliyojiwekea, Chuo kinatekeleza majukumu makuu matano (5) kama ifuatavyo:

i) Kutoa mafunzo katika fani za Sayansi za Jamii kwa kiwango cha Astashahada, Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili;
ii) Kutoa mafunzo ya uongozi (Leadership);
iii) Kufanya utafiti katika nyanja mbalimbali za masomo;
iv) Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa sekta ya umma na sekta binafsi; na
v) Kuendesha mafunzo ya elimu ya kujiendeleza (Continuing Education).

**4. Mafanikio katika Miaka miwili ya Serikali ya awamu ya sita**

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mh. Dkt. Samia Suluhu Hasan Rais wa Jamhuri ya Tanzania, imefanya jitihada mbalimbali katika kuendeleza Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ili kukiwezesha kuwahudumia watanzania kwa mafunzo, utafiti na ushauri wa kitaalamu. Aidha, chuo kimepata mafaniko makubwa katika kutekeleza majukumu mahususi kama ifuatavyo:

(i) Katika Kampasi ya Kivukoni, Chuo kimeboresha miundombinu katika mabweni ya Wanafunzi, madarasa pamoja na ofisi za Wafanyakazi, ikiwa ni pamoja na kuweka umeme jua kwenye mabweni na kwenye barabara, kukarabati nyumba za Wafanyakazi na kanteeni na kuboresha mfumo wa majitaka.

(ii) Katika Kampasi ya Kivukoni kazi ya ujenzi wa maktaba kubwa yenye uwezo wa kuchukua watu zaidi ya 2,500 pamoja na ukumbi wa mihadahara wenye uwezo wa watu 1000, ujenzi unaendelea vizuri upo asilimia 30. Fedha iliyotumika ni Bilion 2.

(iii) Katika Kampasi ya Karume, kazi ya ujenzi wa mabweni yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 1536 inaendelea. Fedha zilizotolewa na serikali ni Bilion 2.

(iv) Katika kampasi ya Pemba, kazi ya ujenzi wa madarasa na jengo la Utawala itaanza mwanzoni mwa Aprili 2023. Bilion 2.6 imetengwa kwa ajili ya ujenzi.

(v) Sera ya Uthibiti Ubora imehuishwa ili kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa ni bora na yenye viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

(vi) Chuo kimeendelea kutumia mtandao wa wireless (WIFI) na kuimarisha utumiaji wa mtandao kwa kuongeza kasi ya mtandao kutoka 36mbps hadi 236mbps;

(vii) Zoezi la kuandaa mitaala mipya na kuhuisha mitaala ya zamani limekamilika ili kuwa na mitaala inayozingatia mahitaji halisi ya kitaifa na kimataifa. Katika

# TANGAZO

maboresho hayo somo la uongozi, maadili, na uzalendo limeingizwa katika Mitaala yote ili kila mwanafunzi awe na ufahamu wa kutosha kuhusu uongozi, maadili, na uzalendo.

(viii) Chuo kimetenga bajeti kwa ajili ya kuwawezesha wahadhiri kufanya tafiti mbalimbali zenye maslahi kwa Chuo na taifa kwa ujumla na tayari wahadhiri wamejengewa uwezo wa kuandika maandiko ya utafiti na machapisho.

(ix) Chuo kimefanikiwa kutoa mafunzo ya Uongozi na Maadili kwa viongozi na watendaji kutoka Taaisisi mbalimbali pamoja na wanafunzi wa Chuo, na kufanya idadi ya waliofuzu mafunzo hayo kuwa zaidi ya 4,000.

(x) Kumekuwa na ongezeko la idadi ya programu za mafunzo ambapo kwa sasa zimefikia Programu 32. Programu hizo ni kwa ngazi ya Astashahada (Cheti), Stashahada (Diploma), Shahada za Awali na Shahada za Umahiri.

(xi) Udahili umeogezeka kutoka wanafunzi 11,413mwaka 2020/2021 hadi 14,457 mwaka 2022/2023.

(xii) Chuo kilifanya mahafali ya 17 katika Kampasi ya Kivukoni tarehe 25/11/2022 ambapo wanafunzi 5,869 walihitimu na kutunukiwa vyeti katika ngazi ya Astashahada ya Awali, Astashahada, Stashahada, Shahada na Shahada ya Umahiri. Aidha, Kampasi ya Karume na Pemba walifanya mahafali ya 7 tarehe 28/11/2022 iliyofanyika katika Kampasi ya Karume ambapo wanafunzi 1,537 wa Kampasi ya Karume na 126 Kampasi ya ya Pemba walihitimu na kutunukiwa vyeti katika ngazi mbalimbali.



PROFESA SHADRACK MWAKALILA
MKUU WA CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE

(xiii) Chuo kimewezesha wahadhiri 56 kwenda kwenye mafunzo kwa ngazi mbalimbali za masomo ikiwemo Shahada ya Uzamivu, Shahada ya Umahili, Shahada ya Awali na Stashahada.

(xiv) Chuo kimefanya mafunzo kupitia semina ya mbinu za ufundishaji kwa wahadhiri wote wa Kampasi zote.

(xv) Chuo kimeongeza idadi ya walimu/wahadhiri wenye shahada ya uzamivu (PhD) kutoka wahadhiri 37 kwa mwaka 2020 hadi wahadhiri 46 mwaka 2023.

(xvi) Idadi ya watumishi imeongezeka baada ya kupata kibali cha ajira za wahadhiri 86 na kufanya jumla ya watumishi wa kudumu kuwa 305,

(xvii) Chuo kimekuwa na bunifu zaidi ya bunifu 22 na zimeshindanishwa kwenye maonesho mbalimbali ambapo kati ya bunifu hizo bunifu moja ilishika nafasi ya pili kitaifa katika mashindando ya maonesho ya Kitaifa ya Sayansi Tekinolojia na Ubunifu (MAKISATU) na Nyingine ilishika nafasi ya nne kitaifa. Bunifu zilizoshinda kitaifa ni kama ifuatavyo:

a) Mfumo wa Umwagiliaji wa kiotamatiki
b) Mfumo wa kugundua uvujaji wa gesi kweny mitungi ya gesi ya kupikia.
c) Mfumo wa kufuatilia na Kupima Joto na Hewa ya Matairi ili Kuzuia Kupasuka kwa Tairi

(xviii) Chuo kimepata Mafanikio katika eneo la Michezo, ambapo Wanafunzi wamekuwa wakishiriki katika mashindano ya SHIMIVUTA yanayohusisha taasisi za elimu ya juu Tanzania kila mwaka na Wafanyakazi wameshiriki mashindano ya SHIMMUTA ambayo hujumuisha Wafanyakazi kutoka Sekta/Taasisi Mashirika ya Umma na Taasisi/Sekta binafsi ambayo pia hufanyika kwa kila mwaka.



MOJA YA HOSTELI ZA WANAFUNZI ILIYOPO CHUONI.




MUONEKANO WA NJE WA MOJA YA UKUMBI WA MIHADHARA WA BENJAMIN MKAPA, KATIKA CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE (1)

TANGAZO

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA)

MAKALA MAALUM

# SERIKALI INAVYOTATUA CHANGAMOTO YA UPATIKANAJI WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA KATIKA MKOA WA DODOMA

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) ilianzishwa mwezi Julai, 1998 kwa mujibu wa kifungu na. 3(1) cha Sheria na. 8 ya mwaka 1997 ambayo ilifanyiwa mabadiliko kwa Sheria na.12 ya mwaka 2009 pamoja na Sheria na. 5 ya mwaka 2019 ya Usambazaji maji na Usafi wa Mazingira.

Jukumu la msingi la DUWASA ni kutoa huduma endelevu ya usambazaji Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa wakazi wa Jiji la Dodoma. Aidha, kwa mujibu wa Muongozo wa Usimamizi wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira wa Desemba 2019, DUWASA inatoa huduma kwenye miji ya Bahi, Chamwino, Kongwa na Kibaigwa (ambayo imeongezwa hivi karibuni)

**Hali ya Huduma ya maji katika maeneo ya utendaji ya DUWASA.**

**Hali ya Huduma ya maji katika Jiji la Dodoma.**
Jiji la Dodoma lina wakazi 765,179 kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya 2022, ambapo takribani asilimia 91 wanapata huduma ya maji safi na salama kwa njia za migao. Migao hii inatokana na ongezeko la mahitaji ya maji ambalo kwa sasa ni lita milioni 133 wakati uwezo wa uzalishaji ni lita 67.1 hivyo kuwa na upungufu wa 50% unaopelekea migao ya maji.

Ilikufikia asilimia 100 ya usambazaji majisafi kwa jiji la Dodoma Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) inaendelea kutekeleza mipango mbalimbali.

Mipango hii imewagawanyika katika maeneo manne (4) ambayo ni, Mpango wa muda mfupi, wakati, mrefu na mpango wa dharula.

Mipango ya muda mfupi ni uchimbaji wa visima maeneo ya pembezoni, ambapo tayari visima vimechimbwa katika maeneo ya Nzuguni, Nala, Ihumwa, Iyumbu, Miyuji na Ntyuka Chimalaa. Hivi karibuni eneo la Nzuguni DUWASA imechimba visima 5 vyenye uwezo wa kuzalisha lita milioni 7.6 kwa siku.

"Mradi huu wenye gharama ya bilioni 4.8 utahusisha pia ujenzi wa miundombinu ili kuyafikisha maji hayo haraka kwa wakazi wapatao 37,000 wa Nzuguni, Ilazo, Swaswa na Kisasa na kuboresha hali ya upatikanaji wa maji Jijini Dodoma". Alisema Mhandisi Aron

"Mradi huu utaongeza uzalishaji wa majisafi kutoka wastani wa lita milioni 67.8 mpaka milioni 76.3 kwa siku, sawa na ongezeko la 11.4% ya uzalishaji wa sasa. Ongezeko hili linapunguza na kukidhi 11.7% ya mahitaji ya sasa ya Jiji lote la Dodoma ambayo ni lita milioni 133 kwa siku. Utekelezaji wa mradi huu umeanza ambapo wazabuni mbalimbali wameshaingia mkataba na DUWASA kuanza utekelezaji. Mikataba hii imesainiwa tarehe 7 Februari 2023. Alisema Mhandisi Aron

Mpango wa dharura ni kutoa maji Bwawa la Mtera na kuyaleta Dodoma ili kutosheleza mahitaji ya maji kwa jiji na maeneo ya pembezoni kwa sasa hadi mwaka 2032. Upembuzi wa awali umeonesha kuna uwezekano wa kutoa hadi kiasi cha lita milioni 130 kwa siku na utagharimu sh. bilioni 326. Na sasa mradi upo hatua ya usanifu.

Mpango wa muda wa kati ni ujenzi wa Bwawa la maji la Farkwa wenye gharama takribani sh. bilioni 312.08 katika awamu ya kwanza, ambazo zimetolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Utekelezaji wa Mradi huu umeanza, na upo hatua ya usanifu.

Lengo la Mradi huu ni kutoa maji Bwawa la Farkwa Wilaya ya Chemba na kuyaleta Dodoma ili kutosheleza mahitaji ya maji kwa jiji na maeneo ya pembezoni kwa sasa hadi mwaka 2042 na chanzo hiki pamoja na kuhudumia eneo la Chamwino, Bahi na Chemba, kinatarajiwa kuongeza maji kiasi cha lita milioni 128 kwa siku kwenye Jiji la Dodoma.

Hata hivyo serikali imeweka mpango wa muda mrefu ikiwa ni kuchukua maji kutoka Ziwa Victoria ambapo upembuzi wa awali uliofanyika na kukamilika mwezi Desemba, 2019 umeonesha uwezekano wa maji ya ziwa Victoria kuja Dodoma upo. Wizara ya Maji inaendelea na hatua za kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

Mji wa Serikali (Mji wa Magufuli) DUWASA tayari imeingia Mkataba na Mhandisi Mshauri kampuni ya Norplan Tanzania (Ltd) kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu. Mradi huu utatekelezwa kwa mwaka mmoja na utanufaisha Mji wa Serikali na baadhi ya maeneo jirani.

Hali ya maji katika mji wa Chamwino
Hali ya upatikanaji wa maji katika mji wa Chamwino imeongezeka kutoa 42% mpaka kufikia 87%. Ongezeko hili limetokana na utekeleza wa miradi mikubwa ya ujenzi wa miundombinu ya maji kama vile ujenzi wa tenki kubwa la lita milioni 2.5 eneo la Buigiri, uchimbaji wa visima 11 na kuongeza mtandao wa maji kutoka km 67 mpaka km 216 kwa sasa. Hii imepelekea ongezeko la uzalishaji maji, ongezeko la wateja na mapato kwa Mamlaka kutoka shilingi milioni 15 hadi kufikia shilingi milioni 70 kwa mwezi.

Pia Wizara ya Maji inaendelea na maandalizi ya utekelezaji Mradi katika Miji 28 (Mji wa Chamwino), ambao utatekelezwa kwa kupitia fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya EXIM India.

"Mnamo tarehe 6/6/2022 Serikali ya Tanzania ilisaini mikataba na Wakandarasi wa miradi hiyo ambayo itajengwa kwa mfumo wa kusanifu na kujenga (design and build). Utiaji saini huu ulifanyika Chamwino-Ikulu na kushuhudiwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania". Alisema Mhandisi Aron
Tayari Mkandarasi kampuni ya Mega Engineering kutoka India ame kabidhiwa eneo la mradi (site possession), na sasa yupo uwandani (site) anaendelea na kazi ya survey kwa ajili ya usanifu.

**Hali ya Maji katika Mji wa Bahi.**
Hali ya upatikanaji wa maji katika Mji wa Bahi imeongezeka kutoka 37% hadi 95%. Hii imetokana na uwekezaji mkubwa wa Serikali Katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maji kwenye mji huu, ambapo mradi wa uchimbaji visima 3, ujenzi wa tenki kubwa la kuhifadhia maji la lita laki 2 na kuongeza matandao wa maji kutoka kilomita 22.5 hadi kufikia 32.6 kwa sasa umekamilika.

**Hali ya maji katika Mji wa Kongwa.**
Katika kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Kongwa Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 841 kuboresha huduma ya maji katika mji wa Kongwa. Baada ya utekelezaji wa miradi mbalimbali upatikanaji wa maji imeimarika na kuongezeka kutoka 44% hadi 88%. Ongezeko hili limesababishwa na utekelezaji wa miradi ya kuboresha huduma kama kutafuta vyanzo vipya maji kwa kuchimba visima vyipya 6 na kuboresha chanzo cha maji cha Sagara, ujenzi wa tenki la kuhifadhia maji na kuongeza mtandao wa maji safi kutoka km 88 hadi km 116 kwa sasa.

**USAFI WA MAZINGIRA**
Kwa upande wa majitaka Serikali imetoa shilingi Bilioni 4.9 kwa ajili ya ukarabati wa mtandao wa majitaka katika eneo la Area C na D. Mradi huu u nahusisha kubadilisha mabomba chakavu ya zege na kulaza mabomba mapya ya plastiki (PVC) kwa umbali wa kilomita 19.

Mradi huu unaotekelezwa na kampuni ya Shanxi Construction Engineering ltd ulianza kutekelezwa mwezi Julai, 2021 na mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Aprili mwaka huu. Kukamilika kwa mradi huu kutaondoa adha ya harufu kali, kufurika na kutapakaa mara kwa mara kwa majitaka katika maeneo hayo.

"Mpaka sasa jumla ya kilometa 18 kati ya kilomita 19 za mabomba ya kipenyo cha 300mm yamelazwa na kufukiwa pia chemba 700 kati ya 1,005 zimejengwa na kukamilika hivyo kufanya mradi kufikia 93.7 za utekelezaji wake". Alisema Mhandisi Aron

Pia Serikali ya Korea imefadhili mradi wa ujenzi wa mtandao wa majitaka usiopungua kilomita 250 na ujenzi wa mabwawa 16 ya kutibu majitaka na kuunganisha wateja takribani 6,000 Jijini Dodoma kupitia Benki ya Exim - Korea kwa mkopo wenye masharti nafuu wenye thamani ya shilingi Bilioni 161.

Usanifu wake umekamilika kwa asilimia 100 na kiasi cha shilingi milioni 611 kimelipwa na DUWASA kama fidia kwa wananchi katika eneo la mradi (Nzuguni) na DUWASA ipo katika hatua za mwisho za kumpata Mhandisi mshauri.

**MAFANIKO**
Uzalishaji maji umeongezeka kutoka wastani wa lita milioni 61.5 na kufika lita milioni 67.8 kwa siku hivyo kuongeza masaa ya usambazaji maji kutoka masaa 5 mpaka 13. DUWASA imeweza kuongezeko idadi ya wateja wa majisafi kutoka 54,124 na kufikia 72,795.

Mamlaka imefanikiwa kupunguza upotevu wa maji kutoka wastani wa 39.1% na kufikia 28.3% na makusanyo ya maduhuli kutoka wastani wa shilingi bilioni 1.6 na kufikia shilingi 2.3 kwa mwezi.

# 12 wafariki tetemeko la ardhi Ecuador

**EL ORO,** ECUADOR

OFISI ya Rais wa Ecuador imesema takribani watu 12 wamefariki katika tetemeko kubwa la ardhi lililotokea usiku wa kuamkia jana kusini mwa nchi hiyo na kwamba liliathiri pia nchi jirani ya Peru.

Taasisi ya Marekani ya Seismological (USGS) ilibainisha kuwa ukubwa wa tetemeko hilo ulikuwa umefikia 6.8.

Ofisi ya Rais wa nchi hiyo ilisema kati ya watu 12 waliofariki 11 ni wa mkoa wa El Oro na mmoja katika mkoa wa Azuay na kwamba tetemeko hilo pia lilijeruhi baadhi ya watu na kusababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu.

Mamlaka nchini humo ilieleza kuwa kitovu cha tetemeko hilo kilipatikana katika mji wa Balao katika kina cha kilomita 44.

Tetemeko hilo la ardhi lilizua taharuki miongoni mwa wakazi walioingia barabarani na kwamba nyumba ziliporomoka katika miji kadhaa, ikiwa ni pamoja na Cuenca, mojawapo ya miji iliyoathirika zaidi.

Magaly Escandón, muuzaji wa cherehani katika jiji la Andean, aliliambia shirika la habari la AFP "Nilitoka barabarani kwa sababu niliona watu wakikimbia, wakiwa na hofu, wengine wakishuka kwenye magari".

Pia AFP iliripoti kuwa katika kituo cha kihistoria cha Cuenca, nyumba za zamani ziliharibiwa na kwamba baadhi ya mashuhuda walisema tetemeko hilo lilisikika huko Quito, Manabi na Manta.

Katika ujumbe wa Rais wa Ecuador Guillermo Lasso, kupitia mtandao wake wa kijamii wa Twitter, alitoa wito kwa wananchi wa taifa hilo kuwa watulivu.

Hata hivyo ilielezwa kuwa nchini Peru, ambapo tetemeko la ardhi lilikuwa la ukubwa mdogo, hakuna majeruhi wala uharibifu mkubwa ambao umeripotiwa kufikia jana.

Kwa mujibu wa Taasisi ya Oceanographic na kikosi cha Jeshi la Wanamaji la Ekuado, tetemeko hilo halikidhi masharti ambayo yanaweza kusababisha tsunami katika Pasifiki.

**RFI**



Rais wa Uturuki, Recep Erdogan, akitangaza kuongezewa muda kwa makubaliano ya usafirishaji wa nafaka kutoka Ukraine, yaliokuwa yamalizike Machi 18. **PICHA: MTANDAO**

# Mpango usafirishaji nafaka za Ukraine waongezewa muda

**KYIV,** UKRAINE

UMOJA wa Mataifa (UN) na Rais wa Uturuki, Recep Erdogan, wamesema mpango wa wakati wa vita unaoruhusu usafirishaji wa nafaka kutoka Ukraine umeongezewa muda wake, licha ya kutobainishwa wazi kuwa umerefushwa kwa muda gani.

Mpango wa wakati wa vita unaoruhusu nafaka kutiririka kutoka Ukraine kwenda mataifa barani Afrika, Mashariki ya Kati na Asia, umeongezewa muda ili kupunguza baa la njaa katika mataifa hayo, ambayo bei za vyakula zinazidi kupaa.

Naibu Waziri Mkuu wa Ukraine, Oleksandr Kubrakov, aliandika ujumbe katika mtandao wake wa twitter kwamba mpango huo umeongezewa siku 120 urefu ambao Ukraine, Uturuki na UN walikuwa wanataka.

Inaelezwa kuwa hakukuwa na maoni ya mara moja kutoka Russia, ambayo ilitaka kufanya upya kwa siku 60.

Aidha, huo ni urefushaji wa pili wa mikataba tofauti ambayo Ukraine na Russia zilitia saini na UN na Uturuki kuruhusu chakula kuondoka katika eneo la Bahari Nyeusi baada ya Russia kuvamia jirani yake zaidi ya mwaka mmoja uliopita.

Ukraine na Russia ni wauzaji wakuu wa kimataifa wa ngano, shayiri, mafuta ya alizeti na bidhaa nyingine za bei nafuu za chakula ambazo mataifa yanayoendelea yanategemea.

Vita nchini Ukraine vilisukuma bei za vyakula juu hadi kuweka rekodi ya kupanda mwaka jana na kuchochea mzozo wa chakula duniani pia unaohusishwa na athari za janga la COVID-19 na sababu za mabadiliko ya tabianchi kama ukame.

Usumbufu huo wa usafirishaji wa nafaka zinazohitajika kwa ajili ya chakula kikuu katika maeneo kama Misri, Lebanon na Nigeria ulizidisha changamoto za kiuchumi na kusaidia kuwasukuma mamilioni ya watu zaidi katika umaskini au uhaba wa chakula.

Inabainishwa kuwa mataifa maskini ambayo yanategemea chakula kutoka nje kwa bei ya dola yanatumia zaidi huku sarafu zao zikidhoofika.

Mpango wa Chakula Duniani wa Umoja wa Mataifa, unasema mgogoro huo umewaacha takriban watu milioni 345 wakikabiliwa na uhaba wa chakula.

UN ilisema mpango wa nafaka wa bahari nyeusi umesaidia kwa kuruhusu tani milioni 24 za nafaka kuondoka kwenye bandari za Ukrainia, huku asilimia 55 ya shehena zikielekea katika mataifa yanayoendelea.

Inaelezwa kuwa mikataba hiyo pia imekabiliwa na vikwazo tangu iliposimamiwa na UN na Uturuki, na kwamba Russia ilijiondoa kwa muda mfupi mwezi Novemba kabla ya kujiunga tena na kuongeza muda wa makubaliano hayo.

Ukraine na baadhi ya maofisa wa Marekani wameilaumu Russia kwa kupungua kwa mtiririko wa meli, jambo ambalo nchi hiyo inakanusha.

Wakati mbolea imekwama, Russia imekuwa ikiuza nje kiasi kikubwa cha ngano baada ya mauzo hayo kushuka kwa kiwango kilichoweka rekodi.

Takwimu kutoka taasisi ya data za kifedha ya Refinitiv zinaonyesha kuwa ngano ya Russia imeuzwa zaidi ya mara mbili hadi tani milioni 3.8 mwezi Januari ikilinganishwa kipindi sawa na hicho mwaka uliopita kabla ya uvamizi.

Kwa mujibu wa Refinitiv, usafirishaji wa ngano ya Russia ulikuwa wa kiwango cha juu au karibu na Novemba, Desemba na Januari na kuongezeka kwa asilimia 24 zaidi ya miezi mitatu iliyopita.

Pia ilikadiria kuwa Russia ingeuza nje tani milioni 44 za ngano mnamo 2022-2023. **DW**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Arumeru**
**Kituo cha KING'ORI**
**Mkoa ARUSHA**
**Shauri la Madai?Ndoa Na..........**
**Jina la mdai ROSE SAMWEL FETT**
**Jina la Mdaiwa HEINZ FETT**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanunu ya 18 ya kanunu za Utaratibu Madai katika Mahakama za Mawnzo)**

Kwakuwa Mdai/Mdaiwa ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba (*eleza hapo habari za madai*) **FIKA MAHAKAMANI KUJIBU WITO HUU**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 14 mwezi 03, Mwaka Saa 4:00 asubuhi/Mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hilini lazima kuleta shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyousu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe **07, Mwezi wa 03 Mawka 2023**



**IN THE DISTRICT MAGISTRATE COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No.25 of 2023**
**In the matter of the estate of the late of the late KUWAYAWAYA STEPHEN KUWAYAWAYA**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by LUCRESIA HUBERTH LYIMO.**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 29 Day of 3, 2023

Dated at Dodoma this 17 day of 3, 2023

RESIDENT MAGISTRATE



**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**FLORA KILATO LUHANGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 967 CQN – SUZUKI KERY.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **KW/RB/891/2023.**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1084 NYONGEZA YA 5 KANUNU YA 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**ARUSHA MJINI**
**Usimamizi wa Mirathi 74/ 2023**

**Ombi la GRACE ELIAS MANDAH kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu RUHIZA HAJI KITARINGO wa KITETO**

**Kwa yeyote anayehusika na mirathi hii popote alipo**

Watu wote wanaodai kuwa na utambulisho wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe **04/04/2023** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani unaweza kukaguliwa.

# DIAMOND AWEKA REKODI AIRTEL KUJIUNGA NA TEKNOLOJIA YA ESIM

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa kizazi kipya, Naseeb Abdul maarufu Diamond Platinum, ambaye ni balozi wa Kampuni ya Airtel, ameweka rekodi baada ya kuwa mteja wa kwanza wa Airtel kujiunga na teknolojia mpya ya eSIM.

eSIM (laini inayounganishwa moja kwa moja na simu) - ni laini ya kidigitali ambayo inamwezesha mteja kutumia laini hiyo kwa matumizi yale yale ya mwenye laini ya simu halisi.

Airtel Tanzania imefanya uzinduzi wa eSIM mwishoni mwa wiki na kuwa kampuni ya kwanza mkononi kuzindua laini ya kidigitali eSIM.

Akizungumza jijini Dar es Salaam baada ya kusajili laini yake kuwa eSIM, Diamond alisema ni furaha kuona Airtel ikileta teknolojia mpya hapa nchini ambayo itasaidia kuondokana na usumbufu wa kutembea na simu zaidi ya moja kutokana na kumiliki laini za simu zaidi.

"Ukiwa na eSIM unaweza kutumia hadi laini tano tofauti kwenye simu moja. Hii ni teknolojia ya kisasa na nachukua fursa hii kuwapongeza Airtel Tanzania kwa ubunifu huu," alisema Diamond.

"Laini ya eSIM ni salama zaidi kwa kuwa huwezi kupoteza laini hiyo bila kupoteza simu yako kwani wote tunafahamu laini za kawaida kuna muda huwa zinapotea, kuibiwa na kutumika kwenye utapeli," alisema Diamond na kuongeza kuwa ikiwa wewe ni mtu wa kusafiri mara kwa mara nje ya nchi eSIM itakuwa ni rahisi kwako kubadilisha mtandao ukiwa popote.

Mkurugenzi wa Mawasiliano Airtel, Beatrice Singano, alisema laini ya kidigitali eSIM inafanya kazi kama zingine za kawaida kama vile kupiga na kupokea simu, ujumbe mfupi wa maneno na huduma zingine zote kama zile za Airtel Money.

"Si kila simu zina uwezo wa kutumia eSIM. Baadhi ya simu zinakubali matumizi ya eSIM ni pamoja na Iphone, Samsung, Goggle, Pixel na Motorola," alisema.

Singano alisisitiza kuwa faida kubwa ya kuwa na eSIM ni suala la usalama, kwamba huwezi kupoteza laini hiyo bila kupoteza simu yako na kuna ugumu wa mtu kucheza na taarifa ukiwa na eSIM.

Alisema kuwa taratibu za kujiunga na eSIM ni zile zile za kusajili laini ya kawaida kwani utatakiwa kuthibitisha alama za vidole pamoja na kuwa na kitambulisho cha NIDA.

"Mteja atatakiwa kufika kwenye duka lolote la Airtel na ataweza kuongozwa jinsi ya kujisajili kwenye mfumo wa kidigitali wa eSIM," alisema.

## 'SAMAKI MKUNJE'...



Watoto wakiandaliwa kuwa wachezaji bora wa baadaye katika mazoezi yanayoendelea viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Timu za Ligi Kuu Z'bar zakiona FA

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU za Ligi Kuu Zanzibar zimeendelea kufanya vibaya katika michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), maarufu FA Cup inayoendela hapa visiwani hapa ikiwa imefikia hatua ya 32-bora.

Hadi kufikia sasa jumla ya timu tano za Ligi Kuu zimeaga mashindano hayo na kushindwa kufuzu hatua ya 16-bora baada ya kupokea vichapo kutoka kwa timu za Ligi za Mikoa na Ligi Daraja la Kwanza Kanda.

Timu za Ligi Kuu ambazo zimeaga mashindano hayo ni Bingwa Mtetezi, Kipanga FC pamoja na Zimamoto FC, Taifa Jang'ombe, Polisi FC pamoja na timu ya Malindi SC.

Timu ambazo zimesonga mbele hadi sasa kutokea Ligi Kuu ni Kundemba FC, Mafunzo SC, Black Sailor, Dulla Boys pamoja na JKU SC ambazo zimefanikiwa kutinga hatua ya 16-bora.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ZFF, Ali Bakar 'Cheupe', alisema kwa msimu huu timu za madaraja ya chini zimekuwa na mwamko zaidi kwa kucheza kwa ushindani pale zimapokutana na vigogo vya Ligi Kuu.

Alisema ushindani huu unatoa changamoto kwa klabu za juu kutodharau mchezo hasa pale wanapocheza na zile za madaraja ya chini.

Cheupe alisema klabu za Mikoa na Kanda zimeonesha ushindani mkubwa ikilinganishwa na ilivyozoeleka katika mashindano hayo hasa katika hatu kama hii.

Aidha, alisema kwa ujumla mashindano hayo yanaendelea kama yalivyopangwa kwa Unguja na Pemba katika viwanja mbalimbali.

Hata hivyo alisema kwa mujibu wa ratiba hatua ya 32-bora itamalizika leo Jumatatu na kuzipata timu 16 ambapo hatua hiyo ya 16-bora itachezwa baada ya kumalizika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Kwa mujibu wa Kanuni ya Kamati ya Mashindano ZFF, mshindi wa michuano hiyo kwa Kanda ya Unguja atacheza na mshindi wa Kanda ya Pemba ili kupata bingwa atakayeiwakilisha Zanzibar katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

# Mradi wa Utanzania ni Nini wazinduliwa Dar

**Na Joseph Mwendapole**

MRADI wa Utanzania ni Nini unaoendeshwa na Kampuni iitwayo OnaStories umezinduliwa jijini Dar es Salaam ukiwa na video zinazoelezea kuhusu Utanzania ni nini mila na tamaduni zake.

Mradi huo uliozinduliwa mwishoni mwa wiki una kazi zinazofanywa na Kampuni ya Media Innovation Center kupitia mradi wa 'Aga Khan Media Innovation Center,'ambapo Onastories walishinda mwaka 2020.

Akizungumza kwenye uzinduzi wa mradi huo, mwanzilishi mwenza wa OnaStories pamoja na mwendeshaji wa mradi huo, Princely Glorious, alisema maonyesho hayo ni matokeo ya mradi ambao wamefanya kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Aga Khan ambao waliwapa msaada wa Dola za Marekani 20,000 mwaka 2021.

Aliendelea kusema, "mradi huo endelevu umekamilisha awamu mbili ambazo ya kwanza ilikuwa ni ukusanyaji wa taarifa, utafiti, kuandaa makala, vibonzo na video elezi katika sehemu kuu tatu upande wa Mavazi (Kaunda Suti), Lugha (Kiswahili) na Muziki (Singeli) na awamu ya pili ni pamoja na kuzindua na kuwasilisha kazi hizo".

Pia mwanzilishi mwenza wa Onastories na mwendeshaji wa mradi huo wa "Utanzania ni Nini?", Tulanana Bohela, alisema, mradi huo umekuwa wenye mafanikio makubwa na kwamba huo ni mwanzo wa kazi nyingi zitakazokuja ambazo zinabeba dhima nzima ya Utanzania ni Nini?.

Alisema mwendelezo wa mradi huo utajikita zaidi katika kuchunguza kwa undani utamaduni wa Kitanzania na kuuonyesha kwa Watanzania.

Kupitia mradi huo, alisema Watanzania wataweza kufahamu ulimwengu wa muziki wa Singeli ambao ni aina ya muziki unaokuwa kwa kasi na wenye ushawishi mkubwa ambao ulianzia Dar es Salaam.

Pamoja na hayo, alisema Watanzania wanaweza kujifunza kuhusu Kaunda Suti ambao ni mtindo maarufu wa mavazi ambao umekuwa alama ya mitindo ya Kitanzania.

"Na bila shaka watu wanaweza kuzama katika historia na maana ya Kiswahili, lugha inayozungumzwa na watu wengi ambayo inaunganisha watu mbalimbali wa Tanzania," alisema.

Alisema Utanzania unahusu kusherehekea utofauti na utajiri wa utamaduni wa Kitanzania kwa kuangazia mambo mbalimbali yanayoifanya Tanzania kuwa ya kipekee.

## ZISIKUPITE

### HAG KUONGEZEWA MITATU
KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, yupo kwenye nafasi ya kuongezewa mkataba wa miaka mitatu, licha ya mazungumzo kuendelea kuhusu kuuzwa kwa klabu hiyo. ***(Mirror)***

### MESLIER AWANIWA CHELSEA
CHELSEA inataka kumsajili golikipa wa Leeds United raia wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 23, Illan Meslier kipindi cha majira ya joto. ***(Football Insider)***

### DIABY AWINDWA NEWCASTLE
KLABU ya Newcastle United imeonesha nia ya kutaka kumsajili winga wa Bayer Leverkusen, Moussa Diaby, mwenye umri wa miaka 23, na mlinzi wa kushoto wa Uholanzi, Mitchel Bakker, 22. ***(90)***

### MO SALAH HAONDOKI LIVER
WAKALA wa Mohamed Salah, Ramy Abbas Issa, amekanusha uvumi kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, anataka kuondoka Liverpool. ***(90min)***

### FIRMINO KUBAKI ULAYA
FOWADI wa Liverpool na Brazil anayeondoka, Roberto Firmino, mwenye umri wa miaka 31, anataka kubaki Ulaya wakati atakapoondoka hapo Anfield mwishoni mwa msimu huu. ***(Football Insider)***

### VERBRUGGEN NA LIVERPOOL
LIVERPOOL na Manchester United inamtaka golikipa wa Anderlecht, Bart Verbruggen, 20. ***(Het Laatste Nieuws)***

### KUDOS HAIFIKIRII UNITED
FOWADI wa Ghana, Mohammed Kudos, anafikiria zaidi kuisaidia Ajax kutetea taji la Ligi Kuu Uholanzi, kuliko kusikiliza uvumi wa yeye kuhamia Manchester United, na amesisitiza ataingia kwenye mazungumzo ya kurefusha mkataba wake muda muafaka utakapowadia. ***(De Telegraaf)***

### BLAKE ANYATIWA SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur, inamfuatilia winga wa Watford, Adrian Blake mwenye umri wa miaka 17, ambaye mkataba wake unamalizika kipindi cha majira ya joto. ***(Mail)***

### KONE AMULIKWA CHELSEA
KLABU ya Borussia Monchengladbach ipo tayari kumpoteza kiungo, Manu Kone, kipindi cha majira ya joto, huku Chelsea ikiwa miongoni mwa timu zinazomwania mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. ***(Caught Offside)***

### VIEIRA, HENRY WACHUANA
WACHEZAJI wa zamani wa Ufaransa na Arsenal, Patrick Vieira na Thierry Henry, wanachuana kuwania nafasi ya kuwa kocha wa Timu ya Taifa ya Marekani. ***(Goal)***

### KVARATSKHELIA ATAKIWA PSG
KLABU ya Paris St-Germain ipo tayari kulipa hadi pauni milioni 159 kwa Napoli ili kumsajili winga wa Georgia, Khvicha Kvaratskhelia mwenye umri wa miaka 22. ***(Corriere dello Sport)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# GUARDIOLA ASEMA HAALAND ANAJITENGENEZEA MATATIZO

●●● Watu wanatarajia kila mechi atafunga mabao matatu au manne, lazima waseme kidogo, najua hajali...

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema Erling Haaland anajitengenezea "tatizo" kwa sababu kiwango chake msimu huu kimekuwa kizuri kiasi kwamba anatarajiwa kufunga hat-trick katika kila mchezo.

Haaland alifunga mabao nane ndani ya siku tano kwa Manchester City na matatu katika ushindi wa 6-0 dhidi ya Burnley kwenye Kombe la FA Jumamosi, akitokea kufunga mabao matano dhidi ya RB Leipzig kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumanne.

Mshambuliaji huyo wa Norway sasa amefunga mabao 42 msimu huu, ikiwa ni pamoja na hat-trick sita, na Guardiola amesema viwango vya juu vitaleta matarajio makubwa zaidi.

"Huyu jamaa atakuwa na tatizo siku zijazo, watu wanatarajia kila mechi atafunga mabao matatu au manne," alisema Guardiola.

"Lazima watu waseme kidogo, najua hajali, ana mtazamo chanya katika maisha yake, ana matumaini, huwa halalamiki, huwa anajiangalia yeye mwenyewe, kadri tunavyocheza vizuri atafunga.

"Namba zinazolengwa sijui. Tunacheza hivi, Erling atafunga mabao."

City wanaingia kwenye mapumziko ya kimataifa wakiwa katika nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu England na wametinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na nusu fainali ya Kombe la FA.

Kikosi cha Guardiola bado kina nafasi ya kushinda mataji matatu, mara ya mwisho kufikiwa na Manchester United ya Sir Alex Ferguson mwaka 1999, na bosi huyo wa City amekiri kuwa wachezaji wake wamekuwa na kiwango kizuri kabla ya kipindi muhimu cha msimu huu.

"Tuko katika wakati mzuri, bila shaka," alisema Guardiola.

"Sijawahi kuwa na hisia hii kwamba tunaweza kufunga kila kona, mpira wa adhabu tulionao. Nadhani Arsenal itadondosha pointi chache, lazima tushinde karibu kila mechi. Ni heshima kucheza tena na Bayern na nusu fainali kule Wembley. Tuko hai tena katika mashindano matatu.

"Nilikuwa na hisia kwamba wachezaji wanajua hatuwezi kupoteza au imekwisha, hiyo inaleta ubora wetu, huo ndio ukweli."

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
MIRANDES
VERSUS
EIBAR
1 | 3.15
X | 2.95
2 | 2.31

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# IBRAHIMOVIC AWEKA REKODI MPYA SERIE A

**MILAN, Italia**

NYOTA wa AC Milan, Zlatan Ibrahimovic, amewekа rekodi ya kuwa mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi katika historia ya Ligi Kuu Italia, Serie A, kufunga bao.

Hata hivyo, bao lake hilo halikuweza kuwaepusha Milan kuchezea kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa Udinese, Jumamosi na kupoteza matumaini ya mabingwa hao watetezi kumaliza katika nne bora.

Akiwa na umri wa miaka 41 na siku 166, mkongwe huyo wa kimataifa wa Sweden aliipita rekodi iliyokuwa ikishikiliwa na Alessandro Costacurta, beki wa zamani wa Milan, ambaye alikuwa na umri wa miaka 41 na siku 25 alipofunga, pia dhidi ya Udinese, Mei 2007.

Ibrahimovic alikuwa anaanza mara ya kwanza katika Ligi Kuu Italia tangu Januari 23, 2022, baada ya kufanyiwa upasuaji wa goti wa muda mrefu mwishoni mwa msimu uliopita.

Bao lake lilikuwa la kusawazisha kwa timu ya Stefano Pioli muda mfupi kabla ya kipindi cha mapumziko kwenye Uwanja wa Friuli.

Marco Silvestri aliokoa mkwaju wa penalti wa Ibrahimovic, ukaenda chini kushoto kwake, lakini uvamizi wa mchezaji wa Udinese, ulimaanisha mkwaju huo upigwe upya.

Udinese walikasirika, huku Kocha Mkuu, Andrea Sottil, akitolewa kwa kadi nyekundu kwa kupinga kwake, lakini Ibrahimovic hakufunga.

# Conte: Wachezaji wa Tottenham wabinafsi

**LONDON, England**

ANTONIO Conte amewashukia wachezaji wa Tottenham Hotspur baada ya sare ya mabao 3-3 Jumamosi dhidi ya Southampton kwenye Ligi Kuu England.

Spurs waliongoza kwa mabao 3-1 katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa St Mary's, baada ya Harry Kane na Ivan Perisic kutikisa nyavu kwa haraka.

Lakini Theo Walcott na James Ward-Prowse, waliisawazishia Southampton na mchezo kumalizika kwa sare hiyo.

Tottenham wameshinda mchezo mmoja tu kati ya mitano iliyopita ya ligi wakiwa ugenini, na huku wakiwa wamekaa nafasi ya nne, wako pointi mbili pekee mbele ya Newcastle United ambao wamecheza michezo miwili zaidi.

Conte, ambaye mustakabali wake ndani ya Spurs haueleweki kabisa, alisema wachezaji wake ni "wabinafsi".

Aliwaambia waandishi wa habari: "Tatizo tumeonyesha sisi si timu. Sisi ni wachezaji 11.

"Naona wachezaji wenye ubinafsi. Ninaona wachezaji ambao hawataki kusaidiana, ambao hawachezi kwa moyo."



Conte alipendekeza suala hilo katika kikosi chake ni jambo ambalo limeisumbua Spurs tangu muda mrefu kabla hajafika.

"Wachezaji hawataki kucheza kwa ushirikiano. Hadithi ya Tottenham ni hii miaka 20 na hawakuwahi kushinda chochote. Kwa nini?" aliuliza.

"Kosa ni klabu tu au kila kocha anayekuja hapa? Mpaka sasa ninajaribu kuficha hali hiyo. Lakini kuna mechi 10 zimesalia.

"Watu wanadhani tunaweza kupigana? Kupigania nini? Kwa mtazamo huu, roho hii, kujitolea. Nimefadhaika sana."

Conte alisisitiza maoni haya alipozungumza na BBC Sport, akisema: "Tunashinda 3-1 zikiwa zimesalia dakika 15 na nadhani lazima ushinde.

"Sitaki kuongelea kipengele cha ufundi, roho haipo, sisi si timu, ni timu ambayo kila mtu anajifikiria.

"Unapokuwa katika njia hii hilo linaweza kutokea, unapoteza dhidi ya Sheffield United na kutolewa kwenye Kombe la FA na pamoja na Milan katika Ligi ya Mabingwa Ulaya. Sioni maana ya uwajibikaji wa wachezaji.

"Sasa ni vigumu - tunafanya kazi kwa bidii na kundi hili na kusonga katika mwelekeo sahihi. Tunarudi nyuma, naona hali nyingi mbaya na hali nyingi za ubinafsi na wachezaji ambao siwapendi.

"Najua namna ya kuzifunga timu, siku za nyuma nilizifunga timu nyingi, timu za ushindi, nina huzuni kubwa juu ya hili kwa sababu mimi na wafanyakazi tunakaa kila siku kufikiria namna ya kujiboresha.

"Kusema kweli, ni wakati wa kuwajibika kwa ajili yangu, wafanyakazi, klabu lakini pia wachezaji. Wachezaji wanaingia uwanjani, mimi ndiye kocha, sawa nachukua jukumu, wachezaji wanapaswa kuchukua.

"Kilichotokea katika kipindi cha mwisho hakikubaliki na nilijaribu kila wakati kuongea ili kujaribu kuboresha hali na kuhamisha umuhimu wa kuwa timu na kusaidiana, lakini sioni hili."

Y
CHEZA USHINDE KASINO

# RAIS SAMIA: SIMBA, YANGA MAMILIONI YA MABAO YAPO

**Na Adam Fungamwango**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, amezipongeza Klabu za Simba na Yanga kwa kuchangamkia fursa aliyotoa kwa kuahidi Sh. miioni 5 kwa kila bao kitakalofungwa kwenye michuano ya kimataifa ambayo zinashiriki, huku akiwataka wachezaji wa timu hizo kuendelea kufunga mabao kwani fursa inaendelea na pesa bado zipo.

Akizungumza jana kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, wakati wa maadhimisho ya kilele cha miaka miwili ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, iliyoandaliwa na Umoja wa Wanawake wa CCM Tanzania (UWT), Rais Samia alisema ndani ya miaka miwili ya uongozi wa awamu hiyo, michezo imenyanyuka kwa kiasi kikubwa na hii inatokana na umuhimu ambao serikali imeutoa kwenye shughuli za vijana, michezo na wasanii, mila na tamaduni za Mtanzania.

Akizungumzia ushiriki wa Simba Ligi ya Mabingwa Afrika na Yanga kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho, Rais Samia alizipongeza klabu hizo kwa kufanya vema na kuipatia sifa Tanzania.

Wakati timu hizo zikienda kucheza mechi za raundi ya tatu, Rais alitoa ahadi ya Sh. milioni tano kwa kila bao litakalofungwa na timu hizo kwenye mechi zao za kimataifa.

"Lakini nipende kuwapongeza wanangu wa Yanga na Simba, nawapongeza kwa kutumia vizuri fursa niliowapa ya goli moja milioni tano. Wameitumia vizuri sana, kwa hesabu nilizonazo, nadhani Yanga wameshalamba milioni 30 na Simba jana (juzi) walichukua Sh. milioni 35, na huko nyuma nadhani walikula milioni 10, kwa hiyo niwapongeze kwa kuitumia vema fursa hiyo. Na ni imani yangu ile kasi iliyopo miguuni ya milioni tano kwa goli itaendelea kuwapo huko mbele, milioni tano zitakapoondoka," alisema Rais.

Pia alisema pesa bado zipo hivyo waendelee kutupia na hii ni baada ya juzi usiku Simba kushinda mabao 7-0 dhidi ya Horoya AC ya Guinea kuona utani wa mashabiki wa soka uliokuwa ukiendelea kwenye mitandao ya kijamii.

"Niwahakikishie wale waliokuwa wakitania jana. Niliona utani, eti nampigia Msigwa (Gerson) namwambia eti maliza mpira haraka, mimi pesa zimeisha, nataka niwahakikishie mama bado anazo, endeleeni kuweka mpira kwenye wavu, bado zipo, wekeni mpira wavuni, jengeni jina la nchi yetu," alisema na kuzua shangwe kubwa uwanjani hapo. Msigwa ni Msemaji Mkuu wa Serikali ambaye ndiye mara zote huonekana kutoa pesa hizo kwa niaba ya Rais pale timu hizo zinapotekeleza kile walichoahidiwa.

Yanga ilikuwa imepata Sh. milioni 30 kabla ya mechi ya jana dhidi ya Monastir ya Tunisia, Simba ikiwa imelamba Sh. milioni 45, hivyo tayari jumla ya Sh. milioni 75 zimeshatolewa na Rais Samia kwa jumla ya mabao 15 yaliyofungwa na timu hizo.

KIKAPU



Wachezaji wa timu za mpira wa Kikapu, JMK (wenye jezi nyeupe) na Ninaki, wakiwania mpira jana katika michuano ya Shule za Sekondari inayofanyika kwenye viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam. Katika mchezo huo JMK ilishinda seti 42 kwa 33. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Chama kinara wa mabao CAF

INATOKA UK. 24

nawashukuru pia mashabiki wetu kwa kujitokeza kwa wingi uwanjani kuipa sapoti timu yao.

"Malengo yetu yalikuwa kuingia robo fainali na tunamshukuru Mungu tumefanikiwa hilo ndio jambo zuri la kujivunia," alisema Robertinho.

Aliongeza kuwa kila mchezaji ndani ya kikosi amefanya majukumu yao mazuri, Kanoute, Chama, Baleke, Mohamed Hussein na Shomari Kapombe walifanya kile alichowaagiza katika uwanja wa mazoezi kwa kukitekeleza uwanjani.

Kocha Msaidizi wa Horoya AC, Sekou Soumah Diego, alisema wamepokea matokeo hayo ingawa hayakuwa mazuri kwao kutokana na kuzidiwa na Simba kila eneo.

Alisema katika soka kuna kushinda, kushindwa na kupoteza, na kwamba mipango yao ilikuwa kushinda mchezo huo na hilo halikutimia, hivyo wanarejea uwanjani kujiandaa na mchezo ujao.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Simba, Salim Abdallah 'Try Again', amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa motisha anaoutoa katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho kwa timu za Tanzania.

Try Again alisema kiasi cha Sh. milioni tano anazotoa Rais Samia kwa kila bao linalofungwa kimeongeza morali na kuwafanya wachezaji kujiona wana deni kubwa kwa nchi.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 20/03/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 4091 | Kocaelispor vs Pazarspor | 1.17 | 6.23 | 11.42 |
| 14:00 | 5269 | Batman vs Amedspor | 3.88 | 3.00 | 1.97 |
| 15:00 | 2664 | FC Sarajevo vs NK Posusje | 1.55 | 3.62 | 5.58 |
| 16:00 | 2147 | Watford U21 vs QPR U23 | 3.79 | 4.15 | 1.68 |
| 16:00 | 3075 | Sheffield Wednesday U23 vs Birmingham U21 | 2.76 | 3.49 | 2.22 |
| 16:00 | 5696 | Wigan U23 vs Hull City U23 | 2.38 | 3.52 | 2.52 |
| 16:15 | 3275 | Kifisias vs Apollon Smyrnis | 1.80 | 3.11 | 4.46 |
| 17:00 | 1159 | FA Siauliai B vs Be1 NFa | 4.62 | 3.60 | 1.62 |
| 17:00 | 2665 | Charlton U23 vs Bristol City U23 | 2.38 | 3.83 | 2.38 |
| 18:00 | 4626 | Aris Limassol vs AEK Larnaca | 2.42 | 3.16 | 2.85 |
| 19:00 | 4120 | U Craiova SA vs CS Mioveni | 1.71 | 3.35 | 4.81 |
| 19:00 | 4281 | ES Bafing vs Denguele Sport | 2.53 | 2.69 | 3.00 |
| 19:00 | 4391 | Flamurtari vs Din. Tirana | 2.28 | 2.85 | 3.21 |
| 20:00 | 5974 | Sakaryaspor vs Bodrumspor | 2.67 | 3.24 | 2.34 |
| 21:00 | 2815 | Ingolstadt vs Dynamo Dresden | 3.32 | 3.37 | 2.08 |
| 21:30 | 1100 | Defensores Cambaceres vs Sportivo Barracas | 2.03 | 3.01 | 3.64 |
| 21:30 | 1299 | St Truiden U21 vs AS Eupen U21 | 2.15 | 3.53 | 2.85 |
| 21:30 | 1669 | Yupanqui vs Deportivo Laferrere | 3.88 | 2.90 | 2.01 |
| 21:30 | 2018 | Berazategui vs Csyd Liniers | 2.30 | 2.90 | 3.11 |
| 21:30 | 2030 | Kortrijk U21 vs Lierse SK U21 | 1.64 | 4.25 | 3.94 |
| 21:30 | 3177 | Waasland Beveren U21 vs Oostende U21 | 4.40 | 4.10 | 1.49 |
| 21:30 | 5564 | Deportivo Muniz vs Argentino Rosario | 2.90 | 2.85 | 2.47 |
| 22:00 | 1185 | Wolverhampton U21 vs West Ham U21 | 2.03 | 3.57 | 3.05 |
| 22:00 | 2173 | Kmsk Deinze U21 vs Lommel U21 | 3.06 | 3.53 | 2.04 |
| 22:00 | 2304 | Deportivo Riestra vs Villa Dalmine | 2.08 | 3.02 | 3.47 |
| 22:00 | 2785 | Westerlo U21 vs Excelsior Virton U21 | 1.93 | 3.69 | 3.22 |
| 22:00 | 3567 | West Bromwich U23 vs Norwich U23 | 2.12 | 3.90 | 2.42 |
| 22:00 | 4818 | Universitatea Cluj vs Argesul Pitesti | 1.74 | 3.49 | 4.37 |
| 22:00 | 5192 | Fortaleza (COL) vs Llaneros FC | 2.03 | 3.11 | 3.48 |
| 22:30 | 1539 | Uruguay Montevideo FC vs IA Sud America | 2.28 | 2.88 | 3.09 |
| 22:30 | 2625 | US Ancona 1905 vs Cesena | 3.09 | 2.93 | 2.46 |
| 22:45 | 3141 | Stourbridge vs Coalville Town | 3.25 | 3.45 | 1.85 |
| 23:00 | 2004 | Mirandes vs Eibar | 3.15 | 2.95 | 2.31 |
| 23:00 | 2048 | Le Mans vs FC Versailles 78 | 2.21 | 3.14 | 3.19 |
| 23:30 | 3806 | Cusco FC vs Carlos Mannucci | 1.53 | 3.86 | 5.04 |

JUMANNE - 21/03/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 1683 | Univ de Concepcion vs Deportes Iquique | 2.41 | 3.11 | 2.75 |
| 00:00 | 2703 | CSD Barnechea vs Rangers | 2.36 | 3.21 | 2.74 |
| 00:00 | 2822 | Club General Caballero Jlm vs Cerro Porteno | 4.31 | 3.44 | 1.70 |
| 00:00 | 4796 | Barranquilla FC vs Patriotas FC | 3.31 | 3.26 | 2.04 |
| 00:05 | 2693 | Cucuta Deportivo vs Deportes Quindio | 2.28 | 3.00 | 3.05 |
| 00:30 | 3174 | NewellS Old Boys vs San Lorenzo | 2.48 | 2.75 | 3.01 |
| 01:00 | 1338 | Molynes vs Chapelton Maroons FC | 1.98 | 3.00 | 3.30 |
| 01:15 | 2995 | CA Cerro vs CA Fenix | 2.72 | 3.13 | 2.37 |
| 02:10 | 5763 | Atletico Bucaramanga vs Deportes Tolima | 2.54 | 2.99 | 2.68 |
| 02:30 | 1359 | San Marcos vs San Luis Quillota | 2.39 | 3.22 | 2.70 |
| 02:30 | 3450 | Puerto Montt vs CD Santa Cruz | 1.94 | 3.05 | 3.88 |
| 02:30 | 4857 | Tacuary Asuncion vs Resistencia FC | 2.23 | 3.13 | 2.93 |
| 03:00 | 1988 | Deportivo Cuenca vs Cumbaya FC | 1.72 | 3.21 | 4.86 |
| 03:00 | 3172 | Huracan vs Rosario Central | 1.81 | 3.21 | 4.24 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Machi 20, 2023

Nipashe




UKURASA 21

**Guardiola asema Haaland anajitengenezea matatizo**

# YANGA YATINGA ROBO FAINALI SHIRIKISHO

## ●●●Yavunja mwiko wa kumaliza mkiani mwaka 2016 na 2018, Musonda, Mayele wafanya yao...

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya kwanza, timu ya Yanga imefanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya jana kuichapa US Monastir ya Tunisia mabao 2-0, mechi ikichezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Yalikuwa ni mabao ya Mzambia Kennedy Musonda na Mkongomani Fiston Mayele ambaye licha ya kuivusha hatua ya makundi, lakini pia kukwea juu na kuliongoza Kundi D ambalo kwa muda mrefu lilikuwa likiongozwa na Watunisia hao.

Yanga ina pointi 10 sawa na Monastir, lakini imefunga mabao manane na manne ya kufungwa, huku Watunisia hao wakiwa na mabao sita na matatu ya kufungwa.

Katika kundi hilo, pia Real Bamako ikiwa nyumbani nchini Mali ilipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na kufikisha alama tano, hivyo timu hizo mbili hata zikishinda mechi zao za mwisho haziwezi kufikia pointi za Yanga na US Monastir.

Yanga ilishindwa kutinga hatua ya robo fainali mara mbili mwaka 2016 na 2018 ilipofanikiwa kucheza hatua ya makundi Kombe la Shirikisho, lakini ikiishia kukamata mkia.

Mara zote iliishia kupata pointi nne tu, ikishinda mechi moja na kutoa sare moja.

Kwenye mechi ya jana, Yanga ingeweza kuweka rekodi ya kupata bao la mapema katika michuano hiyo, kwani sekunde ya 29 tu, straika wake tegemeo, Mayele akiwa umbali ya takribani yadi 35 hivi, aliachia shuti kali la juu lililoonekana kama halina madhara, lakini lilikwenda na kutua langoni, hata hivyo ustadi wa kipa wa US Monastir, Sadok Yeddes, aliruka juu na kuupangua kuwa kona.

Kwa mara nyingine tena, kipa huyo namba mbili wa US Munastir alifanya kazi ya ziada kama ya kwanza, alipokwenda juu na kupangua shuti la Djuma Shaaban dakika ya 17 ya mchezo.

Beki huyo wa kulia raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo aliufumania mpira uliokuwa umeokolewa vibaya na mabeki wa Watunisia hao, nje kidogo ya eneo la hatari.



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, akishangilia baada ya kuifungia timu yake bao la pili wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya US Monastir kwenye mechi ya Kundi D ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana, hivyo kufuzu hatua ya robo fainali. **MPIGAPICHA WETU**

Yanga ambayo ilikitawala kipindi chote cha kwanza, ilifanya shambulizi lingine dakika ya 27, Mayele aliupounganisha krosi ya Joyce Lomalisa kwa mguu wa kulia, lakini alimlenga kipa Yeddes.

Baada ya kosakosa nyingi, hatimaye Musonda aliandika bao la kwanza dakika ya 32, kutokana na wachezaji wa Yanga kupasiana mpira kutoka katikati ya uwanja, ukamfikia Khalid Aucho, ambaye aliupeleka kwenye wingi ya kushoto kwa Jesus Moloko, naye bila kuchelewa alimimina krosi ya juu, Musonda alitoka nyuma na kuuwahi kuupiga kichwa katikati ya walinzi wawili walioonekana kama wanategeana, mpira ukatinga wavuni.

Wageni walionekana kuanza kufurukuta baada ya kufungwa bao, lakini bado hawakufanikiwa kufanya shambulizi lolote la maana kwenye lango la wenyeji wao.

Mwanzoni mwa kipindi cha pili Yanga iliingia kwa kasi na kufanikiwa kuandika bao la pili dakika ya 58, likiwekwa wavuni na Mayele akiunganisha mpira kwa mguu wa kulia, baada ya kazi mzuri iliyofanywa na Musonda aliyetoka na mpira umbali mrefu akiwalamba chenga walinzi wa US Monastir, kabla ya kumpasia mfungaji.

## Chama kinara wa mabao CAF

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

HUKU mabao matatu (hat-trick)aliyofunga kiungo wa Simba, Clatous Chama katika mechi dhidi ya Horoya AC ya Guinea juzi, yakimwezesha kufikisha manne na kukaa kileleni katika orodha ya vinara wa ufungaji kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Robertinho Oliveira, amesema haikuwa kazi rahisi kushinda 7-0.

Katika mchezo huo uliopigwa juzi Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Simba iliibuka na ushindi huo mnono shukrani kwa Chama aliyetupia hat-trick, Jean Baleke na Saido Kanoute, ambao kila moja alicheka na nyavu mara mbili.

Kwa mujibu wa takwimu za Ligi ya Mabingwa Afrika, Chama anaongoza akiwa pamoja na straika wa Al Hilal ya Sudan, Makabi Lilepo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, ambaye naye pia ana mabao manne.

Mzambia huyo wa Simba bao lingine alilifunga mechi iliyopita Machi 7, mwaka huu katika uwanja huo huo, Simba ikiichapa Vipers ya Uganda 1-0.

Wachezaji wanaofuatia ambao wamefunga mabao matatu ni Hamza Khabba wa Raja Casablanca ya Morocco, Mahmoud Kahraba wa Al Ahly ya Misri, Cassius Mailula na Peter Shalulile wote wa Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini ambao kila mmoja ametupia mara tatu.

Wakati huo huo, mchezaji huyo juzi alizawadiwa mbuzi mmoja na shabiki wa timu hiyo aliyeweka ahadi baada ya kufunga bao kwenye mechi dhidi ya Vipers.

Akizungumza na gazeti hili jana, Robertinho alisema waliwaandaa wachezaji wao kucheza vizuri wakiwa hawana mpira kwa kuwa inapunguza kufanya makosa na kuwasoma wapinzani hivyo kuwa na uwezekano wa kutumia vizuri nafasi walizotengeneza.

Alisema malengo yao yalikuwa kucheza vizuri, kupunguza makosa na kupata ushindi kitu ambacho wamefanikiwa kupata matokeo mazuri katika mchezo huo.

"Kupata ushindi mnono wa mabao 7-0 katika Ligi ya Mabingwa Afrika si jambo jepesi na wala haitokei mara kwa mara, tuliwasisitiza wachezaji wetu kuhakikisha tunacheza vizuri tukiwa hatuna mpira.

"Nawapongeza wachezaji wangu kwa kuweza kufuata maelekezo tuliyowapa,

INAENDELEA UK. 23



9 770856 541002 >